

MBONA UNALIALIA? NENA!



...na katika nyumba ya Bwana. Ni vema sana kuwa hapa, na katika huduma ya Bwana Mungu wetu.

² Sasa, haya daima ni ma—majaliwa kwangu kuja kanisani, lakini kuja kwa Ndugu Junie hapa, kidogo ni majaliwa ya ziada. Nimemjua Ndugu Junior kwa muda fulani. Nami nilifurahi sana kumwona akiingia katika njia hii nzuri ya kale ya Injili, na kutoka nje akilihubiri Neno. Kumwona Bwana akimbariki, nao watu wakimheshimu sana, hilo ni zuri sana.

³ Sasa, ninajua kulikuwako na baadhi ya watu hapa asubuhi ya leo, waliokuwa wameendesha motokaa mwendo mrefu, nao hawana budi kurudi usiku wa leo, kwa kuwa huenda ikawa, labda waende kazini kesho, kwa maili nyingi, huko chini Ohio. Na, ama huko juu Ohio, nilimaanisha kusema. Na kidogo nilipoteza njia zangu; huko juu Ohio.

⁴ Halafu tuliahidi ya kwamba, usiku wa leo, tungekuwa na m—mstari wa maombi. Kwa hiyo hatutaki kuwaweka muda mrefu sana. Kuna joto. Halafu basi kwa ajili ya mstari wetu wa maombi. Lakini tunajua ya kwamba tayari mmebarikiwa kwa uimbaji na chochote mlichofanya. I—imekuwa ni baraka kwenu. Nasi tunamtumainia Mungu sasa kwamba Yeye ataendelea tu kuwa pamoja nasi na kutubariki, na kutupa shauku ya moyo wetu. Sasa mmeweka kila kitu mlichu nacho moja kwa moja katika ibada, usikivu wenu wote, uaminifu wote na unyofu mwezao. Nami nimekuwa katika maombi alasiri ya leo kwa ajili ya ibada usiku wa leo.

⁵ Na, sasa, ninatumaini kurudi na kuwa nanyi tena hivi karibuni. Nanyi nyote mtatutembelea, huko maskanini. Tunajisikia ya kwamba kanisa hili dogo ni kanisa shirika kwa maskani. Hivyo ndivyo lilivyo. Ni kanisa shirika dogo tu, la maskani. Hili, na huko kwa Ndugu Graham, na ujirani. Nasi tunafurahi sana kumtembelea dada yetu mdogo usiku wa leo. Nasi tunatumaini ya kwamba maskini dada huyo mdogo atakua na kukua na kukua awe mama mashuhuri. Nami ninaamini atakua, pia, kwa ne—neema na msaada wa Bwana.

⁶ Kama vile Paulo alivyomwambia Timotheo, “Uwe tayari, wakati ufao, wakati usiofaa; uwe tayari. Karipia—karipia, kemea, kwa uvumilivu wote na Mafundisho. Kwa sababu utakuja wakati watakapoyakataa Mafundisho yenye uzima; ila kwa kufuata masikio... utafiti wa masikio yao, watalimbikiza waalimu...”

⁷ Kwa hiyo tunajua, ya kwamba, Mungu akiwa pamoja nasi ni moja ya mambo yaliyo makuu sana. Nilikuwa chumbani, alasiri

ya leo, nikiomba. Nami nikawazia, “Ni kitu gani kilicho kikuu kuliko kujua ya kwamba umeokoka?” Sasa niambieni tu ni kitu gani kingalikuwa kikuu zaidi.

⁸ Nilimwambia rafiki yangu, Ndugu Evans. Nikasema, “Ndugu Evans, kama ningalikuwa na kitufe kidogo hapa ningaliweza kubonyeza, na nirudi kwenye umri wa miaka ishirini, nami ningekuwa na umri wa miaka ishirini kwa muda wa miaka elfu kumi, na kuwa mfalme wa dunia nzima wala nsizeeke hata kidogo, nidumu tu na umri huo; niwe na kila kitu ulimwenguni, mikononi mwangu mwenyewe, na niishi katika anasa kwa muda wa miaka elfu kumi, kisha nipotee mwishoni mwa miaka elfu kumi. Ama, nibonyeze kitufe kingine, na nife mara moja, nikiwa na Uzima wa Milele.” Nikasema, “Ningebonyeza kitufe cha Uzima wa Milele, bila hata kufikiria tena. Kwa kuwa vipi kama. . .”

⁹ Kisha akageuka, naye akasema, “Kweli. Vipi kama tulikuwa tumeishi miaka elfu kumi, na usiku wa leo, saa mbili ama tatu, miaka yetu elfu kumi ilikuwa imekwisha?” Haya basi.

¹⁰ Kwa hiyo hakuna kitu kilicho kikuu kuliko Uzima wa Milele. Na ni kwa ajili yetu sote. “Atakaye na aje.”

¹¹ Sasa, Mungu hatamwajibisha mtu kwa, kwa sababu yeye ni mwenye dhambi, maana alizaliwa mwenye dhambi. Lakini kile Mungu atakachomwajibishia mtu, ni kwa sababu yeye anabaki mwenye dhambi. Haimbidi kubaki mwenye dhambi, kwa kuwa kuna maandalizi yaliyofanywa kwa ajili ya kuhesabiwa haki kwake kupitia kwa Yesu Kristo. Kwa hiyo tunatumaini, usiku wa leo, kukiweko na wengine ndani ama nje, ambao bado hawajamkubali Kristo, kwamba huu utakuwa ndio usiku ambao jambo fulani litasemwa ama kufanywa, ambalo litawaamsha, kufikia mahali unapojua unamhitaji Kristo.

¹² Halafu basi kama ulimkubali tu kama Mwokozi wako binafsi, wala hujampokea Roho Mtakatifu, ninatumaini ya kwamba usiku wa leo utampokea.

¹³ Ninawaona baadhi ya jamaa wa maskanini hapa. Nitasema hivi kuhusu huyo dada mkubwa. Mnaona? Jambo moja ambalo maskani inahitaji huko juu kanisani mwetu, maskanini huko Jeff, ni kujitolea tena na kujazwa tena kwa Roho Mtakatifu. Kweli. Kila mmoja aende madhabahuni na kuomba mpaka wapate kufanywa upya tena kwa Roho Mtakatifu, kanisa lote lijazwe na Nguvu za Mungu, hilo ndilo tunalohitaji. Sio tu ile maskani kule, bali Mwili wa Kristo, ulimwenguni kote, unahitaji kujazwa tena. Napenda. . .

¹⁴ Daudi alisema siku moja, “Unirudishie furaha ya wokovu wangu.” Sasa, hakuwa ameupoteza wokovu wake, bali furaha yake. Basi inapofikia mahali ambapo siwezi kuifurahia dini yangu, wokovu wangu, kuna kasoro mahali fulani, kwa sababu,

“Ni furaha isiyosemeka na iliyojaa utukufu.” Mmoja wao alisema, “Onjeni muone, Bwana yu mwema. Ni mtamu kama asali mwambani.” Loo, nina furaha sana kwamba nimeionja Hiyo. Bwana ni mwema. Nami ninapenda asali, bali kamwe sijapata kuonja yoyote kama Hiyo. Hiyo ndiyo iliyo nzuri kuliko zote niujuayo.

¹⁵ Sasa tutaharakisha tuingie moja kwa moja katika ibada, tuone kama tunaweza kuliachilia kanisa mapema, ili watu waweze kwenda mahali pao, na pa kuabudia, ama kazini kesho, na nyumbani mwao.

¹⁶ Na sasa tunatarajia mkutano mkuu huko kwenye Pwani ya Magharibi, mara moja. Nasi tunaomba na kusihi tupate maombi ya kanisa hili na watu hawa wote, kuniombea.

¹⁷ Asubuhi ya leo kuna jambo fulani lililotukia. Kamwe sijapata kwenda, angalau, kwenye kanisa dogo, pasipo Mungu kunitendea jambo fulani maalum. Ninapenda tu hilo. Basi asubuhi ya leo, nikiisha kumaliza kuhubiri, kwa utaratibu kabisa, Roho Mtakatifu alishuka miongoni mwetu na kutoa ujumbe kwa Ndugu Jackson, ambao umebaki tu nami, alasiri nzima. Hakika, nitaichukua hiyo kanda, kusudi niweze kuicheza tena na tena, niweze kuupata. Kwa kuwa, hivi majuzi, nimekuwa nikijisikia . . . Mke wangu hapa anajua. Nimekuwa nikimwambia ya kwamba Bwana atanizuru kwa njia fulani, mara moja. Basi huenda ilikuwa ni ujumbe huo asubuhi ya leo, maana umenipa mtazamo mpya. Ulinipa somo ambalo ningependa kulizungumzia kwa dakika chache.

¹⁸ Ningependa kusoma sasa kutoka kwenye Kitabu cha Kutoka, mlango wa 14 na kifungu cha 15.

*Bwana akamwambia Musa, Mbona unanililia mimi?
waambie wana wa Israeli waendeleo mbele:*

¹⁹ Naomba nisome kifungu cha 16, pia.

*Nawe . . . inua fimbo yako, . . . ukanyoshe mkono wako
juu ya bahari, na kuigawanya: nao wana wa Israeli
watapita kati ya bahari katika nchi kavu.*

²⁰ Bwana na aongeze baraka Zake kwenye kusomwa kwa Neno Lake.

²¹ Na sasa hebu tuviinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja kwa ajili ya maombi. Basi ikiwa kuna watu wowote hapa ambao wangetaka kukumbukwa katika maombi haya, na mwifanye ijulikane kwa Mungu kwa mkono ulioinuliwa. Bwana na awajalie shauku yenu.

²² Bwana, sisi sasa, kwa uchaji na kwa heshima na kama mtoto, tunatembea kwenye maeneo matakatifu ya maombi. Tunaweka kando kila mzigo, kila dhambi, kila wazo lituzingalo kwa upesi, tupate kupiga mbio kwa subira katika yale mashindano yaliyowekwa mbele zetu. Basi tunapoingia kwenye

huu mchanga mtakatifu, uliobarikiwa wa maombi, tukijua hili, ya kwamba Yesu alisema, “Ombeni Baba lolote katika Jina Langu, nitalitimiza.” Na pia imeandikwa, “Mkikaa ndani Yangu, nalo Neno Langu ndani yenu, ombeni mtakalo, nanyi mtatendewa.”

²³ Basi tunakuja, Bwana, sio katika jina la kanisa hili dogo, wala katika jina la mchungaji wake, ingawa tunawapenda, wala sio katika jina letu wenyewe, kwa kuwa hatuna kitu cha kutoa kupitia kwake. Bali tunakuja katika Jina hilo litoshelezalo kwa yote la Bwana Yesu, Yule aliyetupa ahadi, ya kwamba kama tukiomba katika Jina Lake, tunaweza kupokea chochote tuombacho.

²⁴ Wala tusingetaka kuomba lolote lililokuwa ni uongo. Tungependa kuomba tu kile kingependeza Kwako. Unazijua hali zetu. Unajua kile tunachohitaji. Unajua kile kanisa hili dogo linachohitaji, na kile kila mtu binafsi anachohitaji. Nasi tungekuomba Wewe, Bwana Mungu, kutupa, kila mtu, tunachohitaji. Jalia Roho Mtakatifu mkuu ashuke kwenye jengo hili na kwenye watu hawa, na kulitakasa kundi hili, kusudi Roho Mtakatifu aweze kupata njia huru kupitia kwa kila moyo hapa, usiku wa leo, kutoka mtoto aliye mdogo zaidi hata aliye mwenye umri mkubwa kuliko wote. Lijalie, Bwana.

²⁵ Mikono hii iliyoinuliwa juu, Wewe hakika kabisa uliona, Bwana. Kama shorewanda hawezi kuanguka mtaani pasipo Wewe kujua, ni zaidi sana vipi Wewe unajua wakati mtoto Wako anapoinua mkono wake kuelekea Mbinguni apate mkate. Tumeahidiwa ya kwamba hatapokea jiwe, badala yake. Tunajua ya kwamba Wewe utawapa mkate wanaomba. Nasi tungeomba, kuwakumbuka wote walio wagonjwa na wanaoteseka.

²⁶ Tuna furaha sana kusikia kutoka kwa Ndugu Rogers, ya kwamba yeye alisema alijisikia vema vya kutosha kwenda kazini. Tunashukuru sana kwa ajili ya jambo hilo, Bwana. Tukiomba kwamba utamponya, kwamba kansa hiyo haitapata na—nafasi, bali itakomeshwa na Damu ya Bwana Yesu. Kwa imani tunaiweka Damu ya Bwana Yesu katikati ya mauti ya kansa na ndugu yetu.

²⁷ Sasa tunawaomba wote walio na haja, kila mahali. Jitwalie Mwenyewe utukufu. Liheshimu Neno Lako, Bwana, kama tulivyolisoma. Na utupe ibada kuu ya uponyaji. Kwa ajili ya utukufu wa Mungu tunaomba hayo, katika Jina la Bwana Yesu. Amina.

²⁸ Kwa ajili ya somo, usiku wa leo, ningetaka kutumia maneno matatu: *Mbona Unalialia? Nena!* Na kwa ajili ya somo, ningetaka kutumia, “Msimamo wa watu kwa waliopakwa mafuta wa Mungu,” kwa muda mfupi tu, labda dakika ishirini, ama thelathini, kisha tutaanzisha mstari wa maombi.

²⁹ Mungu alikuwa amemwita Musa, wito maalum. Naye Mungu anapomwita mtu na kumtia mafuta kwa ajili ya ju—jukumu fulani, Yeye anamtarajia mtu huyo kulitekeleza hilo, kikamilifu. Mungu hataki kumpa mtu agizo, naye asitesite kulihusu. Anamtaka aende mbele moja kwa moja na kufanya yale hasa aliyoagizwa kufanya. Usiangalie kulia wala kushoto, songa tu mbele.

³⁰ Nao wana wa Israeli walikuwa katika utumwa kwa muda wa miaka mia nne, bali Mungu alikuwa ameahidi ya kwamba angewazuru. Naye Mungu hutimiza kila ahadi anayofanya. Hawezi kusema uongo. Yeye ni Mungu. Nao wakati ulikuwa umewadia kwa ajili ya kuzuriwa huku.

³¹ Nami ninaamini, usiku wa leo, kwa mlinganisho, kwamba Mungu alifanya ahadi kwamba angerudi tena. Ninaamini ya kwamba tuko karibu na wakati huo. Asubuhi ya leo, nilipokuwa nikizungunza juu ya somo hilo, karibu ningehisi ule—ule mkondo, tuseme, kule kukaribia kwa Bwana Yesu.

³² Sasa, Musa akiisha kuitiwa kusudi hili, bali yeye alikuwa ni mwanadamu. Mungu alimfundisha miaka themanini kabla ya Yeye kuweza kumtumia; miaka arobaini katika ikulu na miaka arobaini nyikani.

³³ Mungu anaweza kumfunza mtu, imchukue miaka mia moja, kwa ajili ya huduma ya dakika thelathini. Mungu anajua jinsi ya kufundisha.

³⁴ Kile shule zilikuwa zimeweka ndani ya Musa, miaka arobaini, ilichukua miaka arobaini kukitoa. Lakini wakati mmoja Mbele za ule Upako, wakati mmoja Mbele ya kile Kichaka kilichowaka moto, alijua mengi zaidi juu ya Mungu kuliko aliyokuwa amejifunza katika vitabu katika miaka themanini ya maisha yake.

³⁵ Mungu huwafunza watu Wake, kisha anawatia mafuta, anawapa ujuzi, anawapitisha kwenye mafunzo magumu, kushuka kupitia kwenye changarawe za adhabu inayowaka moto, kuwajaribu, kuwapima. Si kwamba tu Yeye hufanya hivyo kwa manabii Wake, bali huwafanyia watoto Wake. “Kila mwana amjiaye Mungu hana budi kurudiwa na kujaribiwa,” kujaribiwa kwa Neno Lake. Mnaona, wakati mfinyo unapokuja, wakati mgumu, hapo unapokabili mauti, je, unaweza kusimama pale juu ya Neno la Mungu, useme, “Mungu alisema hivyo. Hilo latosha”?

³⁶ Basi Mungu alikuwa amemwita mtu kama huyo, naye mtu huyo alikuwa ni Musa. Lakini Musa, zaidi sana kama sisi, kila wakati ilipofikia mahali jambo fulani lilipaswa kufanywa, Musa alipaza sauti, “Ee Bwana, nifanye nini mahali hapa?” Sasa hilo si ni kama vile sisi hufanya? Mungu alikuwa amembariki na kumtia mafuta zaidi kuliko ndugu zake, akampa ujumbe na

huduma ambayo haikuwa imewahi kuwa duniani tangu siku hiyo, hadi siku hiyo. Na, hata hivyo, kila wakati jambo fulani lilipotukia, Musa alimkimbilia Mungu nalo, “Bwana, nifanye nini? Nifanye nini katika kisa hiki?”

³⁷ Kidogo Mungu akachoshwa nalo, ninaamini. Kasema, “Mbona unanililia Mimi? Nena na hao watu na wasonge mbele.” Jamani, kama kuna wakati wowote kamwe ilionekana kana kwamba wanapaswa kurudi nyuma, ilikuwa ni wakati huo, bali Mungu hana kurudi nyuma.

³⁸ Hakuna mahali pa kurudi nyuma, katika Mungu. Endelea mbele. Daktari akisema, “Ni kansa,” endelea mbele. Kama akisema, “Ni TB,” endelea mbele. Kama ibilisi akisema, “Huwezi kuachana na *hili*,” endelea mbele. Kama nyumba yako ikisema utakuwa mlokole; endelea mbele. Kanisa likikufukuza; endelea mbele. Hakuna kurudi nyuma. Endelea mbele.

“Nena, na uendele mbele.”

³⁹ Nena (kitu gani?) Neno Lake, na uendele mbele. “BWANA ASEMA HIVI,” na uendele mbele. Walilie watu.

⁴⁰ Lakini hao watu basi wakaasi na kusema, “Afadhali tungelifia huko chini Misri. Ingelikuwa afadhali kwamba makaburi yetu yangetiwa alama, kuliko kutoka kwa fisi na ndege wala mizoga kuidonoa mifupa yetu katika nyika hili. Kwa nini ukatuleta huku nje?” Wakiisha kuona ya kwamba Mungu alikuwa amemwidhinisha Musa kuwa mtumishi Wake.

⁴¹ Mungu, Mungu anapoingia ndani ya mtu, ama watu, katika kusanyiko, ndani ya mwanamume ama mwanamke, Yeye huthibitisha Uwepo Wake. Mungu huthibitisha kwamba Yupo mle. Kwa kuwa Mungu anapokuja, ishara za kimbinguni huanza kutokea. Mtu huyu anakuwa mtu aliyebadilika. Hawako tena vile walivyokuwa. Dhambi imetoweka kutoka maishani mwao. Hofu na tashwishi zimetoweka, kuvunjika moyo. Wanakuwa imara, thabiti. Waishi wafe, ni Kristo. Hawajali kijacho wala kiendacho. Hakuna kinachowatikisa. Wanasonga mbele.

⁴² Naye Musa akajisumbua na watu, nao watu wakamhangaikia Musa. Ndipo akasema, “Tufanye nini?”

Na, “Endelea mbele,” ndilo lililokuwa jawabu.

⁴³ Sasa wao walisema, “Tuko huku nje katika nyika hili, nayo majeshi ya Farao yanatuandama, wamepiga kambi nyuma yetu tu.” Lakini Musa alijua kumtii Mungu.

⁴⁴ Basi kama Mungu akimtuma mwakilishi, Naye anamtia mafuta mwakilishi huyu, na kumtuma ulimwenguni, watu hawana budi kumtii mwakilishi huyo. Daima imekuwa hivyo, kote katika Biblia.

⁴⁵ Musa aliitiwa kazi hiyo. Mungu alikuwa amesema, katika Neno, Yeye angefanya hivyo. Aliahidi ya kwamba angetuma

ki—kitu kama hicho katika siku hiyo, kuwakomboa. Basi Mungu alitimiza sehemu Yake, akamtuma Musa. Nao wana wa Israeli, kwa sababu tu vikwazo vidogo na kadhalika vilitokea, kuwajaribu, walishindwa kutembea taratibu pamoja na Musa.

⁴⁶ Sasa hilo si ni kama tu leo hii? Tunauona Ujumbe ukitokea. Tunaliona Kanisa likiinuka kufikia mahali, juu ya mbawa za Roho Mtakatifu, mpaka Nguvu za Mungu zinamchangamsha kila mtu mle ndani. Utukufu wa Mungu unashuka kote, na ishara na maajabu yanatukia. Chini ya juma moja, Shetani anaruhusiwa kuingia katika kusanyiko hilo. Kwa nini anafanya hivyo? Mungu analiruhusu. Ndipo basi kanisa linaanza kunung'unika, kurudi nyuma. "Labda halikuwa hivyo." Hapo ndipo tunaposhindiwa. Huko ndiko kushindwa kwa kanisa. Haidhuru ni kitu gani kinachotukia, ni Mungu. Endelea mbele.

⁴⁷ "Vema," wasema, "yule pale Ndugu *Nanii*. Nilipiga makelele ya ushindi pamoja naye, lakini amerudi. . ." Haidhuru amefanya nini, hilo halina uhusiano wowote na wewe. "Vema, profesa *nanii* alisema ya kwamba Hilo halikuwa kweli, hilo halikuwa la—la Bwana." Haidhuru profesa alisema nini, wewe ndiye jamaa aliyesimama mahali patakatifu. Wewe ndiye jamaa aliyekuwa kwenye kichaka kilichowaka moto.

⁴⁸ Vipi kama, maprofesa wa Misri, vipi kama Farao angalimwambia Musa, "Loo, unadhanja tu uliona kichaka. Ulidhani ulikuwa na. . .Huo ulikuwa ni mngurumo maskikioni mwako"? Musa alijua mahali aliposimama. Musa alijua ni Nini kilichonena naye.

⁴⁹ Na kila mtu aliyezaliwa kwa Roho wa Mungu, anajua ni kitu gani kinachonena naye hapo Roho Mtakatifu anapokuja. Ananena amani inayopita ufahamu.

⁵⁰ Musa aliitwa. Yeye pamoja na Mungu basi. . .Musa akiisha kupata wito wake, alishuka akaenda Misri. Ndipo hana budi kuwafanya watu kumwamini. Sasa, yeye alikuwa nabii aliyetiwa mafuta wa Bwana, lakini watu hawakumwamini; ingawa Yeye, Mungu, alilithibitisha, kwa ishara na maajabu aliyofanya. Na kwa sababu hawakumwamini Musa, mtumishi wa Bwana, basi walianguka nyikani, na kila mmoja wao akafa, aliyetoka Misri. Hakuna hata mmoja wao aliyeokolewa. Kila mmoja wao alikufa na kuangamia, mbali na Yoshua na Kalebu, walioanza safari, kwa sababu walinung'unika na kulalamika dhidi ya Ujumbe uliothibitishwa ambao Mungu alikuwa ameunena katika Biblia.

⁵¹ Loo, ninapoliwazia hilo! Mungu anapoahidi chochote, Mungu hutimiza Neno Lake. Na wakati Mungu anapolithibitisha Neno hilo kwako, basi liamini. Mungu aliahidi, "Katika siku za mwisho, Yeye angeimwaga Roho Yake juu ya wote wenye mwili. Nao vijana wenu wangeona maono, wazee wataota ndoto. Na juu ya wajakazi Wangu na watumishi wanawake nitaimwaga Roho Yangu. Na kuonyesha ishara

mbinguni, na duniani, na ishara kuu na maajabu yangefanyika katika siku za mwisho.” Na sisi hapa katika siku za mwisho, naye Mungu analitimiza Neno Lake. Roho Mtakatifu yuko hapa, na Yeye anakuthibitisha kule Kuja kwa Bwana Yesu. Nao watu wanamkataa, na kumnung’unikia, kama vile tu ilivyokuwa. Huo ndio ukombozi wetu.

⁵² Musa alikuwa u—ule ubao wa kuonyesha ukombozi wa Israeli, kulingana na Neno la Mungu. Wakati ulikaribia. Mungu akamtuma Musa. Yeye alikuwa Nuru ya Mungu kwa ajili ya siku hiyo.

⁵³ Na, leo hii, wakati unakaribia. Mabomu ya atomiki yako tayari. Huu ulimwengu utalipuliwa vipande-vipande, hivi karibuni sana, majivu kote duniani, hakuna kitu ila majivu ya volkeno. Wakati umekaribia. Naye Mungu aliahidi ataimwaga Roho Yake na kulitoa Kanisa Lake. Naye Roho Mtakatifu yuko hapa akiwakilisha hilo, kwa ishara na maajabu, akithibitisha ya kwamba Yeye ni Yesu Kristo yeye yule, katika umbo la Roho Mtakatifu, akifanya kazi ile aliyofanya alipokuwa hapa duniani.

⁵⁴ Inawapofusha watu. Injili sikuzote huwapofusha watu wasipoyafungua macho yao. Ama utembe, au inawapofusha watu.

⁵⁵ Naam, kila kisa katika Biblia, hapo Mungu alipomtuma mjumbe, naye huyo mjumbe akapokelewa, kulikuwako na uamsho katika wakati huo. Lakini kama hawakupokelewa, hapakuwapo na uamsho, bali ni machafuko tu yaliyofuata kutokuamini.

⁵⁶ Ndivyo ilivyo siku hizi, si lolote pungufu. Nafikiri, leo hii, ningetaka kumtaja mwanamke ambaye ninamwazia, katika Biblia. Naye alikuwa ni mbaya, kwanza kabisa, ameoza kabisa. Maskini msichana mrembo, jina lake Rahabu. Alikuwa ni kafiri, kwanza kabisa. Naye alikuwa kahaba mtaani. Lakini alisikia kwamba kulikuwako na Mungu, sio sanamu iliyokaa bubu, ama tamko la kanuni za imani; bali Mungu aliyeishi miongoni mwa watu Wake, na akawatia mafuta, na ishara na maajabu yalikuwa yakiwafuata. Alisikia habari zake.

⁵⁷ Siku moja, wawakilishi wawili walikuja Yeriko. Na upesi, yeye akiwa mtaani kama kahaba, akawaita, akawapeleka nyumbani mwake. Kasema, “Wanawafuata.” Ndipo akawaficha.

⁵⁸ Nami ninapenda msimamo wake. Kamwe hakusema, “Nitaamini, nitakapomwona yule Yohua mkuu aliyepakwa mafuta akifanya ishara fulani. Laiti ningalimwona Musa akifanya baadhi ya hizo ishara, ningaliamini.” Lakini alisema, “Nimesikia.”

“Imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno.”

⁵⁹ “Nimesikia kwamba Mungu wa Mbinguni, Yule aliye Mungu halisi, yuko pamoja nanyi nyote. Naye amefanya ishara kuu na maajabu. Aliikausha Bahari ya Shamu. Alileta mapigo juu ya Misri. Tunaona jinsi ambavyo alimgeuza adui akamweka mikononi mwenu, nayo nchi yetu nzima inatetemeka, kwa sababu yake. Ninaomba rehema.”

⁶⁰ Hakusema, “Itanibidi kumwona Mungu huyu, kwanza. Hebu nichukue hukumu yangu na kuchukua yale Maandiko yasemayo juu ya hilo.” Basi, mnaona, kamwe hangelilipata.

⁶¹ Lakini, “Imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno la Mungu,” naye akaamini.

⁶² Ndipo wakati maneno haya yalipoletewa Yoshua. Neno *Yoshua* linamaanisha “Mwokozi,” kama vile *Yesu*. Ninii... Wakati alipomletea Yoshua, mtiwa mafuta wa Mungu, nyumba yake iliruhusiwa kusimama. Ndipo hao watu walipozizunguka kuta za Yeriko mara kumi na tatu, na kupiga baragumu, kila mahali kwenye ukuta huo palianguka, isipokuwa nyumba yake, kwa sababu aliamini kabla hajaona kitu chochote. Alilikubali. Akasema, “Hao ni watumishi wa Mungu aliye Juu Sana, nami nitalipokea kwa msingi wa kulisikia. Ninaliamini.” Imani chanzo chake ni kusikia. Yeye alilisia. Akaliamini. Akalikubali.

⁶³ Pia angalieni, wao walisema, “Funga kamba hii nyekundu uliyotushusha kwayo, ifunge dirishani.” Hiyo “nyekundu” ilinena juu ya Damu ya Yesu, ule upatanisho. Basi kila mahali katika ukuta huo palianguka, isipokuwa nyumba ya Rahabu. Ilikaa juu ya ukuta. Mungu alimheshimu. Na Yeye... Aliona mwujiza mkuu ukifanywa pale kama ilivyokuwa kwenye kule kukaushwa kwa Bahari ya Shamu. Kwa kuwa, mkono wa Yehova ulikuwa juu ya mahali hapo padogo, kupalinda. Alikuwa amelikubali, Mtiwa mafuta wa Mungu. Watumishi wa Mungu walienda kule, waliotiwa mafuta, naye akaliamini. Kabla hajaona miujiza, yeye aliliamini, kwa vyovyote vile, na kulikubali.

⁶⁴ Eliya, nabii wa Mungu, aliyetiwa mafuta. Loo, naam, Mungu alimtia mafuta kuwa nabii. Yeye alikuwa mchungaji Eliya. Sidhani Yezebeli angetaka kumwita hivyo, lakini alikuwa ni mchungaji wake vivyo hivyo tu. Mungu alimfanya mchungaji wake, kwa hiyo alimchukia. Ndipo Mungu akamwambia, kasema, “Panda mlimani ukaketi chini kule. Nimewaamuru kunguru kukulisha. Nitakupa maji unywe kutoka kijito cha Kerithi.” Basi akaketi kule chini.

⁶⁵ Ndipo mfalme akasema, “Nendeni mkamkamate mlokole huyo na kumleta huku chini.” Nao hao askari, wote wana silaha pamoja na amri ya mfalme, wakaanza kupanda kile kilima.

⁶⁶ Naye Elisha labda alisimama juu na kusema kitu kama hiki, “Enyi waungwana, hapa ni mahali patakatifu. Nimeitwa na

Mungu kuwa nabii Wake. Ameniagiza nisimame mahali hapa, na kuutangaza ujumbe Wake. Nao ujumbe nilio nao kwa ajili yenu, ‘Msipakaribie mahali hapa.’” Amina. “Kaeni mbali na hapa, ninyi msiotahiriwa. Hivi hamjasoma wakati Musa mtumishi wa Bwana alipouvuka ule mto, nao wasiotahiriwa wakajaribu kumwiga? Wote walizamishwa. Msipakaribie mahali hapa.”

⁶⁷ “Loo,” wakasema, “maskini mzee huyo bingwa tapeli! Kwani ametoka shule gani? Tutaingia, kwa vyovyote vile.”

⁶⁸ Eliya akasema, “Ikiwa mimi ni mtu wa Mungu, na ushuke moto kutoka Mbinguni na kuithibitisha huduma yangu.” Ndipo yapata wakati huo, moto ukashuka na kuwateketeza hamsini.

⁶⁹ Huenda mfalme alisema, “Radi iliwapiga.” Kwa hiyo akawatuma wengine hamsini, na jambo lile lile likatukia. Kutokuamini.

⁷⁰ Watu wanaodhihaki na kulifanyia mizaha Kanisa lililotiwa mafuta la Mungu aliye hai wataangamizwa siku moja katika kuzimu. Hawatakuwa wakiteketezwa kwa dakika chache tu. Huenda ikawa ni muda mrefu.

⁷¹ Kwa hiyo ni mahali patakatifu. Mtiwa mafuta wa Mungu husimama mahali hapo. Hakuna asiyetahiriwa wala chochote najisi kinachoweza kuingia mahali hapo. Hiyo ni kweli. Kama waigaji wakijaribu kufanya kama wao wanavyofanya, mtaona hivi karibu watakuwa si kitu. Lakini waigaji wanathibitisha nini? Kwamba kuna kilicho halisi. Kuna Mungu aliye halisi. Kuna watu wanaotaka kuninii... Hawaliamini, bali wanataka kutenda kana kwamba wanaliamini. Lakini mtu anayemjua Mungu, ni mtu aliyezaliwa tena kwa Roho Mtakatifu na kujazwa na Nguvu za Mungu, akiwa na “BWANA ASEMA HIVI,” na anaendelea mbele. Wanajua jambo fulani limeugusa moyo wao. Wanajua wako sahihi.

⁷² Kwa hiyo Elisha alikuwa ni mtu wa Mungu, aliyetiwa mafuta, ambaye hawakumwamini.

⁷³ Mwangalieni Daudi hapo alipoketi pamoja na Nathani nabii. Daudi, mtu aliyeupendeza moyo wa Mungu, naye alikuwa ndiye mtiwa mafuta. Mungu alimtia mafuta kama mfalme. Daudi hakuwa mfalme tu, bali alikuwa nabii. Kwa hiyo Nathani alikuwa nabii mkuu wa hilo taifa. Daudi alikuwa, takriban, mshairi na nabii, mtunga nyimbo, mwanamuziki. Nao unabii kweli, katika asili yake, zaidi sana ni kama wi—wimbo, wanapotabiri.

⁷⁴ Basi, siku moja wakati nabii pamoja na mfalme walipokuwa wameketi pamoja, Daudi alisema, “Si haki kwangu kuishi katika nyumba ya mwerezi, nalo sanduku la Mungu wangu, chini ya hema.”

⁷⁵ Nami ninawatakeni msikilize, yale maneno muhimu sana ya Nathani. Yeye alisema, “Daudi...” Loo, msikose kulipata

hili sasa, ingieni katikati ya mistari. “Daudi, fanya yote yaliyo moyoni mwako, kwa maana Mungu yu pamoja nawe.” Loo, jamani, ninapowazia hilo! “Daudi, fanya yote yaliyo moyoni mwako, kwa kuwa Mungu yu pamoja nawe.”

“Mbona unanililia Mimi?”

⁷⁶ Mungu yu pamoja nawe. Nena kisha uendelee mbele. Mungu amekutia mafuta. Endelea mbele. Usisitesite huku, useme *hili, lile*, ama *linginelo*. “Ninapaswa kumwamini Mungu? Nimwamini kwa ajili ya jambo hili?” Mtumainie kwa kila pumzi unalovuta.

⁷⁷ Ilikuwa ni yule Jemadari mkuu Stonewall Jackson, ambaye amekuwa jemadari ninayempenda sana tangu Yoshua. Stonewall Jackson aliulizwa wakati mmoja, “Unawezaje kusimama na watu wachache tu, wakati upinzani ni mkuu hivi?”

⁷⁸ Hivyo ndivyo alivyopata jina lake la “Stonewall.” Asingeweza kujongea. Hakujua kurudi nyuma. Tungeweza kumsifu kwa lipi mtu kama huyo? Mtu, wakati Mayankii waliposhuka kwa maelfu, naye akasimama pale katika uchache, bali wasingeweza kumsogeza. Alisimama kama ukuta wa mawe. Hao wengine wote wa jeshi la waasi walikuwa wamerudi nyuma! Ryans akaja, kasema, “Kwani Jackson ana shida gani? Kwa nini yeye haendi?” Akasema, “Yeye anasimama kama ukuta wa mawe.” Hapo ndipo alipopata jina lake.

⁷⁹ Hao majemadari wengine wakamwuliza, kasema, “Bw. Jackson. . .” Jamaa mdogo sana, mwenye nywele nyeusi na macho ya bluu, ana urefu wa futi tano na inchi mbili tu, jamaa asiye na majivuno kabisa, jamaa mdogo mpole wa maneno. Kasema, “Bw. Jackson, unawezaje kustahimili, upinzani kama huo?”

⁸⁰ Kidogo ni mwenye haya, akapiga teke ardhi kwa buti lake. Akasema, “Kamwe sinywi maji pasipo kumshukuru Mungu kwake kwanza.”

⁸¹ Hapo ndipo lilipo. Hakuna kurudi nyuma katika Mungu. “Nena na uendelee mbele.” Hiyo ni kweli. Hilo ndilo agizo la Mungu kwa Kanisa Lake. Hatuna wakati wa kuzembea.

⁸² Wao wanasema, “Uamsho umekwisha.” Haujaisha. Endelea mbele. “Pentekoste imepitwa na wakati.” Sivyo. Ni wakati wa pentekoste kusimama katika Jina la Yesu Kristo na kuendelea mbele. Hakuna kurudi nyuma. Hakuna kukaa mahali pale pale. Hebu tusonge mbele pamoja na Roho, la sivyo Roho ataendelea na mtu mwingine na kukuacha umesimama. Wewe mfuute.

“Fanya yote yaliyo moyoni mwako, kwa maana Mungu yu pamoja nawe.”

⁸³ Wakati Yesu alipokuja: Biblia ilisema, Petro alisema, “Kwenye Siku ya Pentekoste, Yesu wa Nazareti, Mtu aliyethibitishwa na Mungu miongoni mwenu, (vipi?) kwa

ishara, miujiza, na maajabu, ambayo alifanya katikati yenu nyote. Kwa kuwa ninyi nyote, wenyewe, ni mashahidi wa jambo hili.” Yeye alikuwa ni nini? Alikuwa Mtu aliyefanya ishara, aliyetiwa mafuta. Mahali pengine lilisema, “Yesu wa Nazareti, Mtu aliyethibitishwa na Mungu miongoni mwenu.” Uthibitisho wa Mungu ulikuwa juu Yake. Yeye alimthibitishaje? Kwa ishara, maajabu.

⁸⁴ Yesu akasema, “Nisipozitenda kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi. Lakini nikizifanya kazi za Baba Yangu, basi aminini hizo kazi, iwapo hamwezi kuniamini Mimi kama Mwanadamu.” Kwa maneno mengine, Yeye alisema, “Ikiwa hamwezi kuamini mimi—mimi Ndimi, mtaangamia katika dhambi zenu. Bali msiponiamini Mimi, angalau aminini kazi nizifanyazo.” Loo, Yeye alithibitishwa na Mungu, kwa ishara.

⁸⁵ Nikodemo alilielezea vema, alipokuja usiku. Naye akasema, “Mwalimu mwema, tunajua ya kwamba Wewe ni mwalimu uliyetoka kwa Mungu.” Amina. Wasingeweza kulificha. “Tunajua ya kwamba Wewe ni mwalimu uliyetoka kwa Mungu, kwa maana hakuna mtu awezaye kufanya mambo uyafanyayo Wewe, kazi uzifanyazo Wewe, isipokuwa Mungu yu pamoja naye.” Walitambua ya kwamba alithibitishwa na Mungu, akatiwa mafuta na Mungu. Yeye alikuwa ni mtumishi wa Mungu.

⁸⁶ Ilibidi kanisa kutambua hilo, ingawa walimchukia. Walimwita ibilisi. Walijaribu kupata kila namna ya udhuru. Lakini ilipofikia kukabiliana na mambo yalivyo, wao waliamini ya kuwa alikuwa ndiye Mtiwa mafuta, bali waliwazia mengi zaidi juu ya mapokeo yao kuliko walivyowazia juu ya upako wa Mungu.

⁸⁷ Wanaume na wanawake siku hizi watajiunga na matabaka ya kijamii kanisani, wajiunge na kundi fulani la wenye akili, kwa sababu wanapenda kuingia kwenye sehemu za wenye akili, wakati wanajua ya kwamba Roho wa Mungu yuna Uzima na hutenda kazi. Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Na jinsi alivyokuwa wakati huo, hivyo ndivyo alivyo sasa, na atakuwa milele. Naye Mjumbe wa Mungu yuko hapa, Roho Mtakatifu. Kumkataa ni mauti, kumpokea ni Uzima. Kuthibitishwa! Watu wanalikubaliye?

⁸⁸ Sasa, Roho Mtakatifu anao Ujumbe mmoja, “Nena Neno. Endelea mbele.” Hiyo ni kweli. “Usinililie Mimi. Hilo hapo Neno. Linene na uendelee mbele,” BWANA ASEMA HIVI. Huo ndio Ujumbe wa Roho Mtakatifu.

⁸⁹ Sasa hao watu wakaanza kunung’unika. Wakaanguka. Hatutaki kunung’unika.

⁹⁰ Kazi alizofanya Yesu ni zipi? Yeye alisema, “Kazi zangu zinanitangaza Mimi. Kazi Zangu zinathibitisha kwamba mimi ni Nani. Kazi Zangu zinanithibitisha Mimi.”

⁹¹ Mungu alipomtuma Musa, kazi zilimthibitisha. Mungu alipomtuma Eliya, kazi zilimthibitisha. Mungu anapomtia mtu mafuta, kazi zake zinamthibitisha.

⁹² Mungu alipomtuma Roho Mtakatifu katika siku hizi za mwisho, kazi zinamthibitisha. Kujiunga na kanisa, kujiunga na dhehebu, kukubali kanuni ya imani ama fundisho; kama huyo ndiye Roho Mtakatifu, basi sikuzote kumekuwako na Roho Mtakatifu katika kila namna ya dini. Lakini Roho Mtakatifu huyu hana budi kuwa Roho Mtakatifu yeye yule aliyekuwako huko nyuma katika Siku ya Pentekoste, la sivyo si Roho Mtakatifu yule yule. Itambidi kutokubadilika kamwe. Ni Roho yule yule. Hana budi kuishi milele.

⁹³ Yesu alisema, “Kazi nizifanyazo mimi; yeye aniaminiye Mimi.” Yohana Mtakatifu 14:7. “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya. Yeye aniaminiye Mimi!”

⁹⁴ Hakuna mtu anayeweza kuamini Yesu Kristo kuwa ni Mwana wa Mungu mpaka amempokea Roho Mtakatifu. Unalichukua tu kwa imani na kulikubali. Huwezi kusema kwamba ndivyo alivyo. Unaweza kusema, “Ninaamini ndivyo alivyo.” “Lakini hakuna mtu anayeweza kumwita Yesu Kristo mpaka Roho Mtakatifu awe ndani yake.” Biblia ilisema hivyo. Roho Mtakatifu hana budi kuingia, kwanza, ndipo Yeye anatoka ushuhuda. Unajua, wewe mwenyewe, ya kwamba Yesu ndiye Kristo, kwa sababu Yeye anaishi ndani yako. Ndipo Roho Mtakatifu yuyo huyo anajitambulisha Mwenyewe kupitia kwa watu, “Nazo ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.”

⁹⁵ Nalo kanisa linamcheka na kumdhihaki. Tunaishi tu katika siku hiyo. Ma—mazingira yanajiweka tayari kwa ajili ya bomu la atomiki, kwa ajili ya hukumu.

⁹⁶ Kanisa linajiandaa kwa ajili ya Unyakuo. Tunangojea. Matarajio, kungojea! Kanisa linangojea kule Kuja kwa Bwana.

⁹⁷ Ulimwengu unatetemeka, unashangaa ni nani atakuwa wa kwanza kumrushia mwingine bomu. Hatujali ni nani atakayefika pale. Tunaenda *Hapa*, kwa hiyo haijalishi ni nani atakayefika pale. Halina uhusiano wowote nasi.

⁹⁸ Tunashangilia tu, kufurahi, na kuamini ya kwamba siku moja tutasikia sauti kutoka Mbinguni, na hapa Yeye atakuja. Nalo Kanisa Lake litatwaliwa juu hewani, kumlaki na kuwa pamoja na Yeye.

⁹⁹ “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya.”

¹⁰⁰ Petro alisema, “Yesu wa Nazareti, nabii aliyetiwa mafuta, aliyetiwa mafuta na kuthibitishwa na Mungu miongoni mwenu nyote, ambaye ninyi nyote, wenyewe, mnamjua.”

¹⁰¹ Biblia ilisema, pia, ya kwamba, “Mungu alimtia Yesu Kristo mafuta kwa Roho Mtakatifu, hata akaenda akifanya mema,

akiwaponya wagonjwa.” Hiyo ilikuwa ni ishara kwamba Yeye alikuwa kile alichodai kuwa.

¹⁰² Hivyo ndivyo Mungu humtuma. Hivyo ndivyo anavyopaswa kuja katika siku za mwisho. Naye Roho Mtakatifu anayekuja katika siku za mwisho si wa kutuvuta kwenye kanuni ya imani, si kutuvuta kwenye kanisa fulani. Ni wa kutuvuta kwa Mungu, nazo ishara za kimbinguni zinapaswa kumfuata huyo Roho Mtakatifu. Ishara za Roho Mtakatifu ni zipi? Kama Yesu wa Nazareti alikuwa Mtu aliyethibitishwa na Mungu, aliyepakwa mafuta kwa Roho Mtakatifu, hebu tuone alikuwa na Ujumbe wa namna gani. Alifanya nini? Alitenda vipi? Tuone tendo Lake, ndipo tunaweza kuyafuata matendo Yake.

¹⁰³ Tunaona ya kwamba alipokuja kwa mara ya kwanza, kwenye huduma Yake, kwenye umri wa miaka thelathini, wakati alipotiwa mafuta kwa Roho Mtakatifu, jambo la kwanza alilofanya, Yeye alikutana na mtu jina la—lake Petro. Naye akamwambia, kasema, “Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona.” Ndipo akamwamini Yeye.

¹⁰⁴ Kwa nini? Musa alikuwa amenena kabla ya wakati wake, na kusema, “Bwana Mungu wenu atawaondokeshea Nabii kama mimi hasa. Hiyo itakuwa ndiyo ishara. Mtajua. Yeye atakuwa ni Mungu-Nabii. Masihi huyo atakuwa Mungu na Nabii pia, na Yeye atafanya ishara ya Nabii wakati ajapo.”

¹⁰⁵ Kama vile Wayahudi siku hizi. Lewi Pethrus alituma zaidi ya Biblia milioni moja kwa hao Wayahudi, Agano Jipya, waliotoka huko chini katika sehemu zingine za ulimwengu, wala kamwe hawakusikia habari za Yesu. Walikuwa huko chini kwa muda wa miaka elfu mbili mia tano. Wakaanza kusoma hilo Agano Jipya. Ndipo wakasema, “Iwapo huyu ndiye Masihi, tunajua ya kwamba Masihi atakuwa Mungu-Nabii. Iwapo huyu ndiye Masihi, wala hajafa, bali Yu hai tena, na tumwone akifanya ishara ya Nabii. Tutamwamini, kwa kuwa Masihi we—wetu ni Mungu-Nabii.”

¹⁰⁶ Yesu alisema, alipokutana na Petro, Yeye alisema, “Jina lako ni Simoni. Nalo jina la baba yako ni Yona.” Ndipo Petro akaanguka miguuni Pake. Alijua ya kwamba huyo alikuwa ni Yule aliyenewa habari zake. Kabisa wakaenda, wakafuata. . . Filipino akamwendea Nathanaeli na kumwambia kile alichokuwa amepata.

¹⁰⁷ Ndipo Nathanaeli alipokuja mbele Zake, Yeye alisema, “Huyo hapo Mwisraeli ambaye hamna hila ndani yake.”

Kasema, “Rabi, ulinijua lini Wewe?”

¹⁰⁸ Akasema, “Kabla Filipino hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona.”

¹⁰⁹ Akasema, “Wewe ni Mwana wa Mungu. Wewe ni Mfalme wa Israeli.” Walijua Huyu alikuwa ni nani.

Yule Msamaria, wakati aliposema . . .

¹¹⁰ Hapo Yeye aliposema, “Nipe maji ninywe.” Mwanamke huyo, lile taifa la Samaria. Kasema, “Loo, ninii. . .” Kasema, “Nipe maji ninywe.”

¹¹¹ Kasema, “Si kawaida kwenu Wasa- . . . kwenu Wayahudi kuwaomba Wasamaria vitu kama hivyo. Mimi ni mwanamke Msamaria.”

¹¹² Akasema, “Lakini kama ulijua ni Nani uliyekuwa ukisema naye, ungeniomba Mimi maji unywe. Ningekupa maji usije hapa kuyateka.”

¹¹³ Mazungumzo yakaendelea kwa muda, mpaka akaona shida zake zilikuwa wapi. Akasema, “Nenda kamwite mume wako mje naye hapa.”

Akasema, “Sina mume.”

¹¹⁴ Akasema, “Hiyo ni kweli. Umekuwa na watano, na yule unayeishi naye sasa siye mume wako. Ulisema hilo vema.”

¹¹⁵ Akasema, “Bwana!” Loo, ndugu, upesi Roho wa Mungu juu ya mwanamke huyo! “Bwana, naona kwamba Wewe ni nabii. Tunajua kwamba Masihi yuaja, na, ajapo, Yeye atatwambia mambo haya. Lakini u Nani Wewe?”

Akasema, “Mimi Ndiye.”

¹¹⁶ Akaangusha mtungi huo wa maji naye huyo akaenda zake. Alipata kinywaji kutoka kwenye Kisima kilichokuwa kikibubujika nafsini mwake. Akakimbia mjini na kusema, “Njoni, mwone Mtu Ambaye ameniambia mambo ambayo nimetenda. Je, haimkini Huyo kuwa ndiye Masihi?”

¹¹⁷ Huyo alikuwa ni Yeye, jana. Huyo ni Yeye, leo hii. Huyo ni yule yule milele. “Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.” Kwa nini tunakawia? Kwa nini tunashangaa? Je, tunashangaa kama Mungu ataponya ama la? Tumemwona Yeye akiwaponya maelfu, vipofu, wagonjwa, viwete, waliopooza. Wale waliokufa, na kutangazwa wamekufa, walifufuka tena, chini ya nguvu za maombi ya imani. Roho Mtakatifu hufunua, na maelfu wanaponywa, macho yaliyopofuka, masikio yasiyosikia. Ulimwengu unajaribu kulipuuza. Wanajaribu kulitikisa liondoke, bali hawawezi. Linarudi moja kwa moja tena. Liko mbele zao. Huwezi kumtikisa kutoka mikononi mwako.

¹¹⁸ Wakati Pentekoste ilipoibuka kwa mara ya kwanza, miaka arobaini iliyopita, wao walisema, “Haitadumu. Ni kundi la watakatifu wanaojibingirisha.” Ati kudumu? Ndilo kanisa linalokua upesi kuliko yote ulimwenguni. Mwaka jana lilipata waongofu milioni moja na laki tano, ambao ni zaidi ya makanisa mengine yote yakiwekwa pamoja. Milioni moja na laki tano,

mwaka jana. Haya basi. Haiwaki. Ha—haipoi moto. Inawaka, sana. Naam.

¹¹⁹ Wanasema, “Wao wana kichaa.” Wanajaribu kuwatikisa watu waachane nao. Wanajaribu kuwachukua watu, “Ondokeni kwenye kundi hilo. Msijipumbaze nao. Hawana chochote. Achaneni na Huyo.”

¹²⁰ Ni mamoja tu, “Kama nikiinuliwa juu, nitawavuta watu wote Kwangu.” Wakati ishara moja kuu ilipotolewa, ya ubatizo wa Roho Mtakatifu, walinena kwa lugha, na wakaliadini. Mamia na mamia mengi wakamiminika ndani yake. Ndipo ikafikia mahali, wakajaribu kuliondolea hilo mbali, Mungu akasukuma ndani moja kwa moja na kutoa tafsiri juu yake. Ndipo mara walipomalizana na hayo, Mungu akatuma unabii nyuma ya huo.

¹²¹ Akasema, “Akiwako mmoja kati yenu, ambaye ni mjinga, na mtu anene kwa lugha. Lakini kukiwako na mmoja anayetabiri na kusema siri za moyo, basi wote wanaanguka chini na kusema, ‘Mungu kweli yu pamoja nanyi.’” Ni kitu gani? Hiyo hapo ile ishara ya Masihi tena ikiingia. Naam, bwana. Kama mmoja akifunua siri ya moyo, kusanyiko lote litasema, “Kweli Mungu yuko pamoja nanyi.” Ishara ya Masihi, hivyo ndivyo ingekuwa. Tunaona hilo. Kadiri wanavyojaribu kutikisa, ndivyo Mungu atakavyofanya.

¹²² Basi siku moja Yeye atachoshwa na kuwatikisa. Atachoshwa na kulisukuma hilo Kanisa huku na huku. Basi atakapochoshwa, atatosheka, Yeye ataufungulia mfululizo mmoja wa hukumu. Naye ataunyosha mkono wa milele na kulichukua Kanisa Lake. Litaruka liondoke, loo, utukufu, litaruka liondoke asubuhi. Loo, jamani! Ninatamani kuwa kule. Nitakuwako. Kwenye asubuhi hiyo hapo litakapoyachukua mabawa ya asubuhi na kuruka liondoke kwenye mikono ya Mpenzi wake, loo, itakuwa ni siku ya jinsi gani!

¹²³ Leo hii, tunaishi. Kwa nini tuhofu? Kwa nini unashangaa? Kwa nini unangojea? Nena na uendelee mbele. Usilie, useme, “Ee Bwana, je, ni mapenzi Yako kuniponya, leo hii?”

¹²⁴ “Hakika, ni mapenzi Yako.” BWANA ASEMA HIVI, ni mapenzi Yake.

¹²⁵ “Ninaweza kumpokea Roho Mtakatifu leo hii? Siku za miujiza zimepita?” Hakika siku za miujiza ziko hapa, milele. Roho Mtakatifu yuko hapa.

“Je, watu hunena kwa lugha siku hizi?” Biblia ilisema hivyo.

“Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.”

¹²⁶ “Je, watu huufasiri ujumbe?” Biblia ilisema wao huufasiri. Hilo latosha.

¹²⁷ BWANA ASEMA HIVI, nena. Usilie. Nena na uendelee mbele. Mungu hataki kundi la watoto wachanga wanaolialia. Yeye anawataka wanaume walio na uti wa mgongo. Sio mifupa ya matamano, “Laiti ningalikuwa Naye. Laiti ningaliweza kufanya *hili*.” Uti wa mgongo utakaosimama kwenye pengo, amina, udai ushindi, udai wameitwa watoke, katikati ya giza. Haijalishi mtu yeyote anasema nini, tunanena na kuendelea mbele.

¹²⁸ Uaminini Ujumbe. Mungu yuko hapa. Yeye atauthibitisha Ujumbe Wake. Mungu yuko hapa. Yeye ni Mungu yule yule aliyekuwa huko nyuma katika Galilaya. Ni Mungu yule yule aliyekuwa katika siku za Musa. Hawezi kushindwa. Mnaamini hilo? Roho Mtakatifu amekuja, ishara za Roho Mtakatifu.

¹²⁹ Yesu alisema, “Nisipozitenda kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi. Lakini nikizitenda kazi za Baba Yangu, basi niaminini Mimi.”

¹³⁰ Wakati alipomwambia yule mwanamke kisimani, kile kilichokuwa shida yake, yeye alisema, “Huyo ni Masihi.”

¹³¹ Yeye alisema, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya. Na nyingi kuliko hizi atazifanya, kwa maana mimi naenda kwa Baba.” Sasa, la King James linasema “kubwa zaidi.” Ukichukua la asili, halisemi “kubwa zaidi.” Ingewezekanaje kufanya lolote kubwa zaidi? Yeye alikomesha maumbile. Aliwaponya wagonjwa. Akawafufua wafu. Aliwatakaswa wenye ukoma. Loo, Yeye alifanya kila kitu. Lakini akasema, “Mtafanya *nyingi zaidi*. Kwa kuwa sitakuwa tu pamoja nanyi, bali nitakuwa ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari.” Je, mnaamini hilo?

Na tuombe.

¹³² Bwana Yesu, neno moja tu kutoka Kwako litamaanisha zaidi ya yale wahubiri wote ulimwenguni wangeweza kunena. Neno moja tu, Bwana, nena. “Usilie. Nena! Endelee mbele.”

¹³³ Ninaweza kukuona Wewe siku moja ukishuka chini ya mlima. Ulikuwa na njaa. Ukautazama mti mmoja. Ulitarajia kupata matini mle, wala hapakuwapo na matini. Ndipo ukautazama mti huo na kusema, “Kamwe hutazaa matini tena.” Kisha akaondoka.

¹³⁴ Basi kesho yake, yapata aduhuri, walipopitia hapo, huo mti ulikuwa umeanza kunyauka. Ndipo mmoja wa wale mitume, jina lake Petro, akasema, “Utazame ule mti, jinsi unavyonyauka upesi, tangu ulipoulaani.”

¹³⁵ Yeye akasema, “Amin, nawaambia, kama *wewe*, kama utauambia mlima huu, ‘Ng’oka ukatupwe baharini,’ wala usione shaka moyoni mwako, bali uamini ya kwamba yale uliyosema yatatimia, unaweza kupata kile ulichosema.”

¹³⁶ Ee Mungu, ni ahadi ya jinsi gani! Ilitoka kwa nani? Muumba wa mbingu na nchi. “Yeye alikuwa katika ulimwengu, nao ulimwengu uliumbwa Naye, wala ulimwengu haukumjua.”

¹³⁷ Tunakushukuru Wewe, Bwana, kwa ajili ya ahadi hii, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya.”

¹³⁸ Sasa, Baba, katika . . . Kuufuata Ujumbe huu, kama utanena tu, usiku wa leo, kitu fulani katika mkondo wa kimbinguni.

¹³⁹ Ambalo, labda mtu fulani hapa ambaye kamwe hakuwa na fununu ya kwamba Wewe ungali uliishi katika njia hiyo, kwamba wanaamini labda kwamba Wewe ulifufuka, kwamba, “Mahali fulani katika Nchi iliyo mbali sana inayoitwa Mbingu, ya kwamba Wewe unaishi kule na kuliagiza kote, ili upate kanuni zetu za imani na kadhalika.” Ni ujinga jinsi gani kwa mtu kukubali hilo, ni kwa sababu tu hawajafundishwa Biblia.

¹⁴⁰ Wewe ulisema, “Nitakuwa pamoja nanyi hata ukamilifu wa dahari. Nitakuwa ndani yenu, na kazi zile zile nifanyazo ninyi nanyi mtazifanya. Si Mimi nizitendaye hizo kazi, bali Baba anayeishi ndani Yangu.” Uliwaambia wale wanafunzi, “Msiwazie yale mtakayosema. Si ninyi mnenao. Ni Roho aliye ndani yenu, ndiye anayenena.” Loo, jinsi tunavyokushukuru Wewe, Mungu aliye Mtakatifu Sana, kwa ajili ya ahadi hizi! Nina furaha sana kujua hilo!

¹⁴¹ Moyo wangu umechangamka, kujua ya kwamba papa hapa, mimi tayari nikiwa na umri wa miaka hamsini, huku nikiishi hapa katika vivuli vya wakati. Kwenye wakati wa jioni wa maisha yangu, na nikiona wakati wa jioni wa historia ya ulimwengu, karibu na kule Kuja kwa Bwana Yesu, na kujua Ukweli huu mkuu umo kifuari mwangu. Unawaka kama moto. Ni furaha isiyosemeka na iliyojaa utukufu. Kuna juhudi humo inayoita, kuupigia kelele ulimwengu, “Loo, mpokeeni, kabla haijachelewa kupita kiasi.”

¹⁴² Tujalie, Bwana, ya kwamba, usiku wa leo, kwamba ule mfano mkamilifu ambao Kristo alitupa, utarudi kwetu usiku wa leo katika Nguvu za kufufuka Kwake. Tujalie, Bwana, kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

Na . . .

Sasa ingieni katika roho ya kuabudu.

. . . Nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

[Ndugu Branham anavumisha *Nampenda*—Mh.]

¹⁴³ Bwana, Ee Bwana, njoo sasa. Tunakuamini Wewe. Nasi tunakuomba ututie mafuta, mtie mafuta mtumishi Wako, Bwana. Yachukue macho yangu na midomo yangu, nia ya—yangu, akili za—zangu, zitumie kwa utukufu Wako. Nena kupitia mtumishi Wako, Bwana. Sikia kupitia kwa masikio ya hili kusanyiko. Jipe utukufu. Jipatie utukufu kwa Jina Lako, Bwana. Jalia pasiwepo na mtu mnyonge miongoni mwetu, ibada hii itakapokwisha.

¹⁴⁴ Sasa, nimenena, Bwana, kwa hawa watu. Sasa, Wewe nena nasi tutaendelea mbele, kukuamini Wewe, ya kwamba upo hapa pamoja nasi. “Msiogope enyi kundi dogo, Baba yenu ameona vema kuwapa Ufalme.” Tunaamini hilo, Baba. Sasa, ichukue hii ibada, Bwana. Huu ndio umbali ninaoweza kwenda. Itakuhitaji Wewe, tangu hapa na kuendelea, Bwana. Katika Jina la Yesu Kristo, nisaidie. Amina.

¹⁴⁵ [Sehemu tupu kwenye kanda. Ndugu Jackson anatabiri—Mh.] Amina.

¹⁴⁶ Sasa, hiyo inaitwa roho ya unabii, inawaangukia watu mbalimbali. Mnaona? Sasa, Yeye alifanya “ahadi,” alitupa ahadi, hiyo inamaanisha kuwa Yuko hapa. Mnaona? Sasa, Junie ni maskini jamaa mwoga. Hiyo siyo tabia yake kuzungumza namna hiyo, lakini, wakati upako unapokamata, mnaona, ni jambo tofauti basi. Hiyo ni kweli. Hiyo, wakati mwingine, ni Roho wa Mungu anayekata kama upanga wenye makali kuwili, mnaona, na Yeye hufanya mambo. Sasa, tunamshukuru Mungu, kuyaona mambo haya.

¹⁴⁷ Sasa, ninaamini ya kwamba Junie na Billy waliketi hapa muda mfupi uliopita. Hiyo ni kweli?...kuninii, ama, naam, kusambaza kadi za maombi ama kitu fulani. Kasema, “Kuna baadhi ya watu waliokuja.” Nasi tulikuwa tukiwatarajia wengine wachache, labda kutoka nje na kadhalika, lakini walisema hapakuwapo na wengi sana. Kwa hiyo tutawafanyiza mstari wale tulio nao, labda, katika wakati mmoja.

¹⁴⁸ Tutaanzia kwenye namba moja, na kuwapangisha mstari watu wote, na kumwombea kila mmoja wao. Kwa hiyo tutaona kama Bwana atatufunulia lolote, katika mstari wa maombi. Tutaanzia kwenye namba moja, tulipange hili kundi mstarini. Ni nani aliye na kadi namba moja? Waweza tu kuja? [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

Yesu mwenye huruma,
Ananena kufurahisha moyo wenye huzuni,
Loo, isikilizeni Sauti ya Yesu.

Sauti iliyo tamu sana katika wimbo wa
malaika,

Jina lililo tamu kuliko yote kwenye ulimi wa
mwanadamu,
Wimbo wa furaha sana uliowahi kuimbwa,
Yesu, Yesu mwenye heri.

149 Nilikuwa nikiangalia mstarini. Sina uhakika, sidhani
kunaye mtu yeyote pale. . .

150 Msichana huyu anayesimama papa *hapa*, aliongea nami
asubuhi ya leo, na kuniambia alikuwa hapa kutoka mahali
pengine, ya kwamba alikuwa—alikuwa ameponywa wakati
mmoja mikutanoni, bali kamwe hakusema lolote kuhusu
nafsi yake. Alisema tu alikuwa ameponywa wakati mmoja
mikutanoni. Ninaamini hiyo ilikuwa ni kweli.

151 Na huyo jamaa nyuma yake, siamini ya kwamba ninamjua
yeyote wa hao. Ama, mama huyu, sijui.

152 Ninamjua Dada Funk. Huyu *hapa*, huyo ndiye nimjuaye,
papa hapa. Yeye ndiye pekee ninayemjua mle ndani, umbali huu.

153 Sasa, kama mtu yeyote akiingia mstarini, na endapo
ninawafahamu, vema, nitajaribu kutokusema lolote, mwajua,
zaidi ya maombi. Kwa sababu mngewazia ya kuwa hao watu
walikuwa wameniambia.

154 Lakini, sasa, hatujui kwamba Roho Mtakatifu atasema
lolote. Huenda asiseme. Lakini hili hapa kamilifu, kamilifu. . .

155 Ndugu, sasa, kuna jambo moja, ni kusema jambo fulani;
jambo lingine, ni kuliona limethibitishwa. Biblia ilisema,
“Thibitisha yote,” (y-o-t-e) “mambo yote.” Kisha, “Shikilia sana
yaliyo mema.”

156 Sasa, kama Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele,
Yeye habadiliki, basi itambidi kutenda katika Kanisa Lake,
ambapo ni sasa. Ni wangapi wanaojua ya kwamba Kristo ndiye
Roho wa Mungu? Sote tunajua hilo. Yeye ndiye Mtiwa mafuta.
Yesu alitiwa mafuta.

157 Hapo ndipo watu, ambao wanaamini ya kwamba kuna
miungu watatu ama wanne mbalimbali, wanapochanganyikiwa
kabisa. Mnaona?

158 Mungu ni Roho. Yesu alikuwa ni mwili ambao Roho wa
Mungu aliishi ndani yake; akamfanya Imanueli, Mungu ndani ya
maskani duniani. Yeye alikuwa ni Mungu. Yesu Kristo alikuwa
ni Mungu, hata hivyo alikuwa ni Mwana wa Mungu. Mwili
Wake ulikuwa ni Mwana wa Mungu, maana Mungu aliuumba,
lakini, ndani, Yeye alikuwa ni Mungu. “Si Mimi,” kasema Yesu,
“nifanyaye kazi. Ni Baba Yangu anayeishi ndani Yangu.” “Na
siku hiyo, mtajua ya kwamba Mimi niko ndani ya Baba, Baba
ndani Yangu; Mimi ndani yenu, nanyi ndani Yangu.” Haya basi.

159 Sasa, ninaamini ya kwamba mama huyu. . . Simjui. Sidhani ninamfahamu. Kama ninamfahamu, si—si—sikujui sasa. Ni—nimekusahau. Nadhani hiyo ni kweli. Naam. Hiyo ni kweli.

160 Naye mama yule *pale*, siamini ninamfahamu; mama *huyu*, ama *yule*. Sidhani ninamfahamu yeyote mbali na Dada Funk. Kama hiyo ni kama kweli, inueni mikono yenu. Kama mimi. . . Hiyo ni kweli. Vema, bwana.

161 Ni wangapi huko nje wanaojua ya kwamba siwajui, na hata hivyo mu wagonjwa? Inua mkono wako, useme, “Ni—ningetaka maombi. Mimi. . .” Nawe unaamini ya kwamba Roho Mtakatifu angeweza kukugusa, kukufanyia jambo fulani, basi inua tu mkono wako, useme, “Ni—ni—nina haja ya maombi.” Inua mkono wako. Mungu awabariki. Hao watu wawili *hapo*. Mama huyu *hapa*. Vema. Wengine, mama fulani *pale* nyuma. Sasa, haikubidi kuwa hapa juu.

162 Palikuwapo na mwanamke wakati mmoja aliyeligusa vazi Lake. Naye akageuka, kasema, “Ni nani aliyenigusa?”

Na, mbona, wao walisema, “Wote wanakugusa.”

163 Yeye akasema, “Lakini nimekuwa dhaifu. Nguvu zimenitoka.” Akasema, “Nimekuwa dhaifu. Nguvu. . . Naona ya kwamba nguvu zimenitoka.” Ndipo akaangalia pande zote mpaka akampata huyo mwanamke, na kumwambia kuhusu kutokwa kwake na damu.

164 Naye akasema, “Kulikuwa kumekoma.” Hiyo ni kweli? Kutokwa na damu kulikuwa kumekoma, kwa sababu alikuwa amemwamini Yesu Kristo. Ni nzuri jinsi gani! Hiyo ni. . .

165 Naye Yesu Kristo ni Kuhani Mkuu, usiku wa leo, anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Mguse tu. Liamini. Ni wangapi wanaonijua mimi, na hata hivyo unajua sijui shida yako, bali ungetaka Mungu akuponye? Inua mkono wako. Uhuh. Jambo ndilo hilo.

166 Sasa angalieni tu huku, na muamini. Iweni na imani. Sasa, Biblia inadai ya kwamba Yesu ni yeye yule, inadai ya kwamba kazi alizofanya zingefanywa na wale wanaomwamini, hasa sana katika siku za mwisho. Mnaamini tunaishi katika siku za mwisho?

167 Sasa, kumbukeni. Ishara za Mungu, kwa wenye akili, ni upumbavu. Inahitaji wa kiroho kulifunua, kama tu watoto wachanga.

168 Sasa, nabii alisema, “Itakuja siku. . .” Sasa, hiyo ilikuwa yapata miaka elfu mbili mia tano iliyopita. “Kutakuja wakati ambapo haitakuwa usiku wala mchana. Itakuwa ni siku yenye utusitusi. Lakini wakati wa jioni, jua litachomoza, itakuwa Nuru.” Ni wangapi waliowahi kusoma unabii huo? Hakika. “Nuru!”

¹⁶⁹ Sasa hiyo inamaanisha nini? Jua, kijeografia, huchomoza Mashariki na kutua Magharibi. Na mtu yeyote anayejua historia, anajua ya kwamba ustaarabu umesafiri kutoka Mashariki kwenda Magharibi. Uchina ndio ustaarabu wa kale sana tulio nao. Vema. Kutoka Mashariki kwenda Magharibi, ustaarabu umesafiri. Sasa, Mashariki na Magharibi zimekutana. Sisi ndio ulimwengu uliostaarabika sana, inavyodhaniwa. Watu waliostaarabika sana wako katika... watu hawa wa Magharibi. Wao ni wa kisasa zaidi. Wanayo mambo yote ya kisasa, na kadhalika, kwa kuwa ustaarabu umepata maendeleo wakati ukisafiri kuelekea magharibi.

¹⁷⁰ Sasa, ni kitu gani kilichowaangukia watu wa Mashariki? Yesu Kristo alikuja juu ya watu wa Mashariki, naye Roho Mtakatifu akaja kwenye Siku ya Pentekoste. Alionyesha ishara kuu na maajabu, kisha akaondoka.

¹⁷¹ Ndipo ukaja wakati, baada ya yapata miaka 200 baada ya kifo cha Kristo, yapata zamu ya pili ya mitume, ndipo wakaingia kwenye siku ya 300, kulingana na Wazee Waliotangulia Nikea, yale masimulizi ya historia takatifu ya kanisa, ambapo hapo waliunda kile kilichoitwa wa—wazee wa mwanzoni. Nao wakaunda kile kinachojulikana leo hii kama kanisa Katoliki la Kirumi huko Rumi. Kwa hiyo, wakaunda dhehebu lao la kwanza. Nayo Rumi, wakati kanisa Katoliki linaposema ya kwamba hilo ndilo kanisa “mama,” kabisa ndilo mama ya makanisa ya kimadhehebu. Ndilo kanisa la kwanza lililopata kuunda dhehebu.

¹⁷² Miaka mia tano, ilienda katika kanisa Katoliki, mpaka Martin Luther. Alilipinga kanisa Katoliki, kwa kukataa kuuita ushirika mwili halisi wa Kristo, na kuupinga, na kutupa huo ushirika sakafuni. Naye akapewa kitubio, kutambaa kwa magoti yake, naye akakataa kufanya hivyo. Ndipo akaunda lile tunalolijua kama kanisa la Kilutheri. Walikuwa na uhuru wa habari, magazeti na kadhalika.

¹⁷³ Ndipo wakaliundia dhehebu na kuunda dhehebu kama dhehebu la kanisa Katoliki. Hilo likaendelea kwa miaka mia kadhaa.

¹⁷⁴ Moja kwa moja akaja Zwingli. Baada ya Zwingli... Yeye—yeye kidogo alikuwa a—aliyetupwa nje. Aliamini, ya kwamba, “Yesu alikuwa ni Mwana wa Mungu, kiasi kwamba ‘aliitwa’ Mwana wa Mungu; lakini, ni ‘mwana wa Yusufu,’ wala hakuzaliwa Kiungu.” Sasa, Wa—Waswisi walishikilia fundisho la Zwingli.

Kutoka hapo akaja Calvin. Calvin akajitokeza.

¹⁷⁵ Ndipo kutoka kwa Calvin wakaja wengine, mpaka tukampata John Wesley. Yeye alinuka katika siku za kanisa

la Calvinini huko Uingereza, ambalo lilikuwa ni Waanglikana, Waanglo-Saksoni.

¹⁷⁶ Kutokana na hao likaja kundi la utakatifu, ambalo linaitwa Methodisti. Nao walipokuja, wakaunda kanisa lililoitwa kanisa la Methodist. Kutokana na kanisa la Methodist, likatoka kwenye hilo, moja kwa lingine. Ndipo likaja la Presbiteri, na kutoka kwa Presbiteri likaja la—la Baptisti, na la Baptisti hadi kwenye...moja hadi lingine, na kuendelea, kuendelea, kuendelea.

¹⁷⁷ Mpaka, kanisa la mwisho kuundwa ni Pentekoste. Nayo baraka ya kipentekoste iliyoshuka katika mfano wa Roho Mtakatifu, wao wakaiundia dhehebu. Hiyo ni kweli kabisa.

¹⁷⁸ Mungu kamwe hakuliundia kanisa dhehebu, wala siamini alipata kuidhinisha dhehebu. Biblia inazungumza dhidi yake, na kudai, kwamba, “Yule kahaba,” kanisa la Kirumi, “atachomwa moto pamoja na watoto wake.” Hiyo ni kweli kabisa.

¹⁷⁹ Lakini kutoka hapo, “Siku imewadia,” ambayo nabii alisema, “ambayo haikuwa ni usiku wala mchana; yenye utusitusi.”

¹⁸⁰ Wamekuwa na Nuru ya kutosha, wangesema, “Vema, tunazozana. Sisi ni Baptisti. Sisi ni Lutheri. Sisi ni *nanii*. Sisi ndio *lile*,” kwa sababu ya madhehebu, kweli ndogondogo walizopata katika Biblia.

¹⁸¹ Luther aliunda dhehebu juu ya, “Wenye haki wataishi kwa imani.” John Wesley aliundia dhehebu, “Utakaso, kazi ya pili dhahiri ya neema.” Pentekoste iliunda dhehebu juu ya, “Kunena kwa lugha, kama ushahidi wa Roho Mtakatifu.” Mambo hayo yote ni ya kweli. Hiyo ni Nuru, bali si yote. Nawe unapotunga kanuni ya imani, huna budi kudumu na hiyo. Huwezi kusonga. Kwa hiyo, Roho Mtakatifu anaondoka na kwenda mahali pengine, ndipo wanaunda dhehebu. Sasa, hiyo ni historia takatifu hasa.

Lakini sasa umekuja wakati, “Nuru za jioni zimekuja.”

¹⁸² Ustaarabu umekuja huku, na sasa jua linatua juu ya ustaarabu. Mwisho umewadia. Mwisho wa ulimwengu uko hapa. Mwisho wa wakati uko hapa. Mwisho wa kanisa uko hapa. Mambo yote yamefika mwisho. Na kama tu vile jua linavyotua...Jua lile lile linalochomoza Mashariki, hutua Magharibi.

¹⁸³ Mungu aliahidi, “Itakuwa Nuru wakati wa jioni,” kwa nabii. Mwana yule yule aliyechomoza na kumwonyesha Roho Mtakatifu kupitia Yesu Kristo, huko nyuma katika siku za mwanzoni, kwenye upeo wa Mashariki, anaangaza kwenye upeo wa Magharibi, katika siku ya mwisho, akionyesha ishara zile zile ambazo Yesu alitabiri zingekuwako. Ni ninii tu. . . Ni Maandiko,

ewe rafiki. Lakini, wewe, ni juu yako, yale unayowazia juu Yake, unaona.

¹⁸⁴ Huyu hapa mwanamke. Njoo huku, dada, tafadhali. Nijuavyo mimi, sijawahi kumwona huyu mwanamke. Simjui. Yeye ni mwanamke tu, aliyekuja hapa. Huenda akawa ni mshiriki wa kanisa hili. Huenda akawa ni mshiriki wa maskani, kwa yote nijuayo. Sijui. Mwanamke tu, kama nimewahi kumwona kabla ya leo hii, sijui mimi. Sijui.

¹⁸⁵ Bali Mungu anamjua mwanamke huyu. Vema, sasa, ikiwa Yesu ni yeye yule jana, leo, na hata milele, basi yeye yuko hapa kwa ajili ya jambo fulani. Sijui ni nini.

¹⁸⁶ Vipi kama huyu ni kama tu yu—yule mwanamke kisimani? Sio lazima kiwe ni kisa cha aina ile ile, lakini ingeweza kuwa tu ni mwanamume na mwanamke wakikutana kwa njia ile ile. Labda huyu mwanamke ni mkosoaji. Labda ni Mkristo. Labda yuko hapa juu akishuku tu, kujaribu kujua kitu fulani. Labda yuko hapa juu kwa sababu yeye ni mgonjwa. Labda yuko hapa juu, amesimama hapa kwa ajili ya mtu mwingine. Sijui mimi. Hiyo ni kweli. Siwezi kukwambia, bali Mungu anajua. Ndipo mnasema . . .

¹⁸⁷ Hebu tuseme yeye ni mgonjwa, maana ni ibada ya uponyaji. Labda ni mgonjwa; huenda asiwe. Lakini kama yeye ni mgonjwa, naye amesimama hapa apate kuombewa, Mungu anajua sijui lolote kulihusu. Vema, basi, iwapo simjui huyu mwanamke, sijui chochote kumhusu, halafu yeye anamtafuta Yesu, kwa ajili ya uponyaji, ningemwambia hili, kwamba, “Kwa mapigo Yake wewe uliponywa.”

¹⁸⁸ Sasa, uponyaji ni kama tu wokovu. Hupati wokovu usiku wa leo. Wakati Yesu alipokufa, Yeye alilipia dhambi yako. Unaukubali tu. Unaona? Wakati Yeye alipokufa, aliziondoa dhambi za ulimwengu. Hapo alipokufa, Yeye alimponya kila mgonjwa. Deni yote ililipwa.

¹⁸⁹ Sasa, vipi kama Yesu alikuwa hapa usiku wa leo katika mfano wa mwanadamu, kama alivyokuwa wakati alipotembea Galilaya? Vipi kama alikuwa amevaa suti hii na alikuwa amesimama hapa, naye mwanamke huyu alikuwa amesimama karibu hivyo na Bwana wetu? Ninii—ninii . . . Hakika ningependa kusimama namna hiyo, Kwake. Vipi kama huyu mwanamke alikuwa amesimama hapo, na Yeye alikuwa amesimama hapa? Naye angemwambia, “Mwanamke, unaamini kwamba mimi Ndiye? Kama huamini, utaangamia.”

Angesema, “Naam, Bwana. Ninaamini ya kwamba Wewe Ndiye.”

“Vema, unatafuta nini?”

“Ninatafuta uponyaji, Bwana.”

¹⁹⁰ “Mwanangu, hivi huwezi kuamini ya kuwa nilifanya hivyo wakati nilipokufa huko ng’ambo, wakati niliposema imekwisha? Hivi Maandiko hayakuandikwa, yaliyosema ya kwamba nilijeruhiwa kwa makosa yako; kwa mapigo Yangu uliponywa?” Jambo ndilo hilo.

¹⁹¹ Vema, sasa, yeye angeshangaa, “Nashangaa kama huyo ni Bwana? Kwamba Yeye... Mtu yeyote angeweza kusema hivyo. Mtu yeyote angeweza kuhubiri hilo, kwa sababu liko katika Biblia. Lakini ikiwa huyo kweli Ndiye, Yeye angeujua moyo wangu, kwa sababu Yeye alijua moyo wa yule mwanamke kisimani. Naye aliahidi jambo lilo hilo.”

¹⁹² Sasa, Yeye kamwe hakusema angerudi katika umbo la mwili na kufanya hili, bali angemtuma Roho Mtakatifu ambaye angeishi ndani yetu, kwamba Roho huyo Mtakatifu angezitambua siri za mioyo. “Kwa kuwa atawaonyesha mambo yajayo, na kuzifunua siri za mioyo.” Hiyo ni kweli? Yeye aliliahidi. Basi kama Yeye ni yeye yule...

¹⁹³ Nami na—nasema hivi, ya kwamba ninaamini Roho huyu mkuu aliye miongoni mwetu ni Roho Mtakatifu. Ninaamini ya kwamba Yeye aliniita kwa kusudi hili. Hainifanyi mimi zaidi ya mtu aliyeokoka asubuhi ya leo hata kidogo; ni mtumishi wenu tu, ndugu yenu. Inanifanya mdogo zaidi kuliko ninyi, kwa sababu nimetumwa kuwatumikia. Mimi ni mtumishi wa umma.

¹⁹⁴ Utumishi wa umma, ni mhudumu; kuutumikia umma, apate kuwa wa chini, kustahimili mapigo na ugomvi wa umma. Chochote kile, asimame hapo. Basi usipokuwa na neema ya kutosha kutabasamu na kulistahimili, basi inakupasa kurudi Kalvari kuhakikisha tena utume wako. Hivyo ndivyo unavyopaswa kufanya.

¹⁹⁵ Sasa, lakini kama Kristo yuko hapa, basi acheni Kristo anene. Mimi simjui huyu mwanamke. Mungu anajua. Simjui huyu mwanamke. Sijui lolote kumhusu. Lakini kama nimesema kweli, basi Yesu Kristo hana budi kulitetea Neno Lake, kwa maana ni Kweli. Hilo linalifanya kweli? Sisi sote tunaamini hilo. Vema.

¹⁹⁶ Sasa hapa ndipo shindano la kuamua linapokuja. Je, Maandiko ni ya kweli, ama ni ya uongo? Sasa, hapa ndipo... Sio huko nje kwenye vyumba fulani vyenye giza. Sio huko nje ambako ibilisi anafanyia kazi. Ni papa hapa mbele ya nyumba ya Mungu, papa hapa mbele ya watakatifu waliotiwa mafuta na watoto wa Mungu, walionunuliwa kwa Damu Yake. Sisi hapa tumesimama, sote wawili, mbele za Mungu na mbele ya jukwaa hili takatifu, Biblia hii, Roho Mtakatifu akiwepo. Sasa ni jambo gani litakalotukia? Mimi ni mwanadamu, kama vile ulivyo wewe. Sasa, haina budi kuchukua Uungu, haina budi kuchukua Roho la siyo haitafanya kazi. Lakini ninajua kwamba Yeye yuko hapa. Yeye alifanya ahadi. Hawezi kuighairi hiyo ahadi.

¹⁹⁷ Sasa, Bwana, tangu sasa ninaomba ya kwamba Wewe utajidhihirisha Mwenyewe, watu wapate kuona ya kwamba Wewe ni Mwana wa Mungu. Na hili limeruhusiwa na Wewe, kulitimiza Neno kwetu sisi Mataifa. Wayahudi waliliona katika siku zao. Wasamaria waliliona katika siku zao. Lakini Mataifa hawakuliona, kwa sababu lilifichwa kwao. Nawe ulisema wangekuwa na siku yao. Sasa ni wakati wa Mataifa, Nawe unawaonyesha. Iwapo ulijifunua Mwenyewe kama Masihi, kwa Wayahudi, kwa kumwambia Petro alikuwa ni nani, kumwambia Nathanaeli alikuwa ni nani; na Wewe ukajifunua Mwenyewe kwa Wasamaria, kwa kumwambia yule mwanamke kwamba, ile shida aliyokuwa nayo; basi huwezi kuwapita Mataifa, kwa kujiunga tu na kanisa. Hawana budi kupokea ya kimbinguni, kwa sababu Wewe ni yeye yule jana, leo, na hata milele, na Wewe unajitambulisha Mwenyewe vivyo hivyo. Lijalie, Bwana, itakuwa ni hivyo, kulitimiza Neno Lako. Katika Jina la Bwana Yesu Kristo, ninaomba hayo.

¹⁹⁸ Pia, Baba, ninaomba ya kwamba utawalinda hawa watu. Maana, tunatambua ya kwamba ikiwa pepo wachafu wako juu ya wagonjwa hawa, watawaendea wakosoaji au chochote zaidi. Kwa hiyo ninaomba ya kwamba utatulinda na kutupatia rehema sisi sote. Tunaomba katika Jina la Kristo. Amina.

¹⁹⁹ Ninakutaka wewe kujibu tu. Kwanza, ninataka tu kuzungumza na wewe, kama Bwana wetu alivyozungumza na yule mwanamke kisimani.

²⁰⁰ Sasa unasema, “Mbona unafanya hivyo, Ndugu Branham?” Kuishika roho yako.

Kama tu Yeye alivyofanya, alisema, “Nipe maji ninywe.”

²⁰¹ Akaja, akaleta maji, alikuwa akienda kuleta maji. Lakini akasema, “Si kawaida ninyi Wayahudi kuwaomba Wasamaria kitu kama hicho.”

²⁰² Akaanza kuzungumza naye, “Lakini kama ulijua ni Nani uliyekuwa ukisema naye.”

²⁰³ Sasa, juu ya hili, sisi hatufahamiani, tunakutana kwa mara yetu ya kwanza. Basi, wewe uko hapa kwa kusudi fulani. Sijui ni nini. Lakini kama Bwana Mungu atanifunulia kile kilichokuleta hapa, ama kitu fulani ambacho umefanya, kitu ambacho unatazamia kifanywe. Na kama Yeye angeweza kukwambia kile wewe umekuwa, hakika Yeye angejua kile utakachokuwa. Kwa kuwa utajua kama hilo ni kweli ama si kweli. Unajua kama hilo ni kweli, maana wewe ndiwe uliyeishi sehemu hiyo ya maisha. Vema, kama Yeye anaweza kukwambia kile wewe umekuwa, basi anaweza kukwambia kile utakachokuwa, hakika ungejisikia vizuri kufanya hilo, sivyo? Hakika ungejisikia. Kwa hiyo hiyo ndiyo siri yake. Mnaona? Hizo ndizo nguvu zake. Huyu ndiye Roho Mtakatifu, kujifunua Mwenyewe, kama Yeye alivyoahidi.

204 Sasa, wewe ni—wewe ni mwanamke, mimi mwanamume. Tumesimama hapa. Unayo roho, la sivyo usingekuwa umesimama hapo. Mimi ninayo roho; nisingekuwa nimesimama hapa. Naona ya kwamba wewe ni Mkristo. Kwa sababu, mara roho yako inaposhika hapa, inakaribishwa. Roho Mtakatifu, ambaye yuko juu yetu, anakutambua kama mtoto Wake. Sasa, sikuwa na fununu, kama huyo mwanamke alikuwa ni Mkristo, ama ni mwenye dhambi, ama mkufuru, au nini, ila roho huyo!

205 Na sasa kama hili kusanyiko...Ni wangapi waliopata kuona ile picha ya yule Malaika wa Bwana, waliyo nayo huko Washington, DC, na kila mahali? Mnaona? Huyu hapa, papa hapa kati yangu na huyu mwanamke.

206 Sasa, utakubali, ama unajua ya kwamba kitu Fulani kiko karibu nawe, hisia tamu kweli. Hiyo ni kweli. Kusudi watu waweze kujua, inua tu mkono wako, wapate kuona. Ni hisia tamu kweli. Ninaangalia moja kwa moja kwenye Nuru hiyo. Inajongea moja kwa moja kati yangu na huyu mwanamke.

207 Sasa, Nguzo hiyo ya Moto iliwafuata wana wa Israeli, nyikani. Ilikuwa katika kichaka kilichowaka moto, iliyosema na Musa. Wakati ilipowakilishwa katika Mwanadamu, Yesu, Yeye alisema, “Ibrahimu asijakuwapo, MIMI NIKO.” MIMI NIKO Ndiye aliyekuwa katika kile kichaka kilichowaka moto.

208 Nazo zile kazi ambazo MIMI NIKO alifanya, hapo alipokuwa katika Yesu, aliahidi angekuja katika siku za mwisho na kufanya jambo lile lile tena. Hii hapa, Nguzo ile ile ya Moto. Wanasayansi wanaijua. Ulimwengu unaijua. Kanisa linaijua. Sisi tunaijua. Hii hapa. Je, itafanya kazi? Ni kitu kile kile? Hakika. Ni kitu kile kile.

209 Kuna ugonjwa wa damu unaomsumbua mwanamke huyu. Ninaiona hiyo damu, inaonekana kama ni nyembamba ama nyeupe. Loo, ni kisukari. Yeye ana kisukari. Hiyo ni kweli. Simjui huyu mwanamke. Na awe ndiye shahidi. Uchunguzi ulikuwa ukionyesha kitu ambacho kilikuwa ni kisukari. [Dada huyo anasema, “Hiyo ni kweli.”—Mh.] Hiyo ndiyo shida yako. [“Hiyo ni kweli.”] Hiyo ni kweli.

Sasa ninyi mnasema, “Ulibahatisha hilo, Ndugu Branham.”

210 Tutaona kama Yeye alibahatisha. Mbali na hayo, anaugua wasiwasi mkuu mno. Hiyo ni kweli. Una shida miguuni mwako pia. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Si kubahatisha, sivyo? [Dada huyo anasema, “La, bwana.”—Mh.] Hutoki hapa. Umetoka Kusini. Umetoka Texas. Jina lako ni Bibi Christian. Rudi; umeponywa...?...

211 Sasa, sio kubahatisha, sivyo, ewe rafiki? Ni Roho wa Bwana. “Kama unaweza kuamini.”

212 Hebu kidogo. Mnaona? Mnaona? [Dada huyo anashangilia—Mh.] Yeye anashangilia tu sasa, akiwa na wakati mzuri

sana katika Roho. Mnaona? Jambo fulani lilimfanyikia. Laana hiyo ilimwacha huyo mwanamke. Kama ungalikuwa ukiteseka namna hiyo, labda ungekuwa ukijisikia vile vile.

213 Vema, mama. Sasa, je, unaamini ya kwamba Bwana Yesu ni yeye yule jana, leo, na hata milele? [Dada huyo anasema “Ninaamini.”—Mh.] Kama Bwana Yesu atanena kupitia kwangu na kuniambia shida yako, utajua kama ni kweli ama si kweli. Huko hapa kwa ajili yako mwenyewe. Uko hapa kwa ajili ya mtu mwingine, mwanao. Huyo mwanao ana ugonjwa wa pafu, na ugonjwa wa matumbo. Sasa, lesa hiyo uliyopangusa machozi nayo, iweke juu yake. Usitie shaka. Atapata afya. Usitie shaka. Mungu akubariki, dada.

214 U hali gani, mama? Sasa, mwanamke huyu anayesimama hapa ametiwa uvuli wa mauti. Unaamini Bwana anaweza kukuponya? Mungu huponya kansa. Unajua hilo. Kansa ya titi. Hiyo ni kweli. Lakini unaukubali uponyaji wako. Wewe ni Bibi Woodward. Rudi, amini kwa moyo wako wote, itakuacha. Kama ungali unaweza kuamini kama unavyoamini sasa, hutakufa nayo. Mungu akubariki. Nenda zako na kushangilia. Amini.

215 Sasa, mama huyu ndiye, ninaamini, aliezungumza nami asubuhi ya leo, kasema umeponywa mkutanoni hapo awali. Vema. [Dada huyo anasema, “Miaka saba iliyopita...?...”—Mh.] Miaka saba iliyopita. Vema.

216 Songea tu huku, mbali na feni hapo, ukiweza, labda unaweza kunisikia vizuri zaidi. Songea tu huku, karibu tu zaidi kidogo.

217 Basi, ni juavyo mimi, hatufahamiani, si zaidi ya kukuamkua tu “u hali gani,” asubuhi ya leo. Nilikwambia, kama ulihitaji kitu kuhusu upambanuzi, afadhali ungojee hadi usiku wa leo, tupate kukusanyika pamoja chumbani na kumwacha Roho Mtakatifu labda afunue jambo fulani ambalo lingetusaidia.

218 Sasa, wewe ni mgonjwa sana, maana unasimama hapo kwa shida. Nawe u—unataka kuamini. Unajaribu kuamini. Wakati mmoja ulikuwa umetiwa uvuli wa mauti, pia. Hicho kifua kikuu, ama kitu kama hicho, ambacho ulikuwa nacho miaka kadhaa iliyopita. Na sasa una tatizo katika koo lako. [“Naam.”] Nawe unahofu kwamba ni kansa. Unahofu kwamba hivyo ndivyo ilivyo. Unashangaa kama hiyo ni kweli. Pia una-... Unataka maombi. Unaombea jambo fulani, ama mtu fulani aliye nyumbani kwako. Hiyo ni kweli. Unatoka Ohio, Bibi McCarroll.

219 Ee Bwana Mungu, Muumba wa mbingu na nchi, ondolea mbali woga kutoka kwa mtoto huyu. Kama uliyaokoa maisha yake, miaka kadhaa iliyopita, kutokana na kivuli hicho, na kukiona kikiondoka, ingeweza kuwa ni vivyo hivyo usiku wa leo. Ninamhukumu ibilisi huyu; mwache huyu mwanamke, katika Jina la Yesu Kristo. Jalia arudi na awe mzima, ahudhurie

mkutano wa usoni, akitoa ushuhuda wa uponyaji huu. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

²²⁰ Usione shaka hata kidogo. Nenda nyumbani, upate afya. [Dada huyo anasema, “Unafikiri nitakuwa mzima, Ndugu Branham?”—Mh.] Hakika. Ninaamini u mzima. Nenda tu huko nje, ukishangilia, ukisema, “Asante, Yesu.”

“Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana.”

²²¹ Unaamini, bwana? Unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? [Ndugu huyo anasema, “Ninaamini.”—Mh.] Sio...Mtumishi Wake tu, unaona, hebu tuliseme hivyo. Hatufahamiani. Si—sikujui, wala wewe hunijui mimi. Sasa kuna jambo fulani limetukia mahali fulani, jambo fulani limetukia kwenye kusanyiko. La, halikutendeka. Limetendeka tena. Ni mtu fulani unayemwombea, ni mtoto. Hiyo ni kweli. Vema. Ilikuwa ni mtoto. Nilidhani ilikuwa ni mtoto kwenye kusanyiko, bali ni mtoto wako. Loo, kuna mambo kadhaa kasoro. Amepangiwa upasuaji wa ngiri, na kadhalika. Umetoka Illinois. Rudi, kuwa na imani. Mtoto wako atapona. Mungu akubariki. Njoo. Bwana akubariki.

Unaamini? Mwamini Mungu. Usione shaka.

²²² Ninamfahamu mtu huyu anayeketi hapa pembeni. Sijui jina lake, bali ninajua ya kwamba yeye huja hapa. Yeye hushuka, mara kwa mara. Ametoka Michigan. Lakini ameketi hapo, akiomba. Sijui shida yake ni nini, kufikia sasa hivi, lakini ninajua sasa. Kwa hiyo nitamwambia, maana ninaamini itamsaidia. Ugonjwa wako wa mgongo umekuacha...?... Kuwa na imani.

²²³ Unaamini kwa moyo wako wote, bwana? Ni ugonjwa wa damu, kisukari. Nawe pia, hutoki hapa. Unatoka Georgia. Wewe ni Bw. Johnson. Rudi, amini kwa moyo wako wote. Utakuacha.

²²⁴ Sasa, loo, sikujui wewe, siamini. Lakini nilimwona Bibi Scharrer ametokea hapa. Bibi Sharrer yuko jengoni? Loo, yeye anaombea shida ile ile ya mwanamke *huyu*. *Wewe* una ugonjwa wa tumbo, *nawe* una ugonjwa wa tumbo. Hiyo ni kweli. Ni huyo pepo anayejaribu kumshikilia kila mmoja wenu. Mmeponywa. Endeleeni mbele mkapate afya...?...

²²⁵ Huamini hilo, sivyo? Unaamini Mungu atamponya, ampe afya, mvulana mdogo? Unahofu ni TB. Lakini unaamini ya kwamba Mungu ataiponya? Usijali, Dada Funk, itakuwa sawa. Mungu akubariki.

²²⁶ Ni nani mwingine aliye na kadi ya maombi? Angalieni, yapata mmoja ama wawili zaidi, nadhani.

²²⁷ Huyu ni mama yako? Nilimwona amesimama karibu nawe wakati huo. Yeye ana kororo anayotaka iombewe.

228 “Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana.” Mwamini tu Mungu. Yeyote wenu tu, tazameni mpate kuishi. Mnaliamini? Mbona, Kristo yuko hapa.

229 Unajisikia tofauti sasa, sivyo, dada? Sasa nenda nyumbani ukapate afya sasa. Ninii tu. . . [Dada huyo anasema, “Unaamini nitakuwa mzima?”—Mh.] Mbona, hakika. Bila shaka. Bila shaka. Ninaamini umepona. Hakika. Amina. Ninii tu, unaona, wewe, wewe una hicho kinyongo ulichozungushiwa, unaona, bali nguvu zake zimevunjwa, dakika chache tu zilizopita sasa. Endelea tu kuamini. Kaza mwendo tu. Endelea mbele, nena, “Kwa mapigo Yake mimi nimepona.” Kabiliana moja kwa moja nao, nawe utaendelea mbele tu, upate afya. Kila kitu kitakuwa sawa. Inaonekana Nuru imekuzunguka kabisa sasa, mahali palipokuwa na giza wakati ulipokuwa hapa, jukwaani. Uko sawa. Baraka iko juu yako sasa, kama ukiendelea tu kwenda mbele.

230 Jina la Bwana na libarikiwe. Unaamini kwa moyo wako wote? Ninajisikia tu kama Roho Mtakatifu anataka kufanya jambo fulani, lililo kuu sana. Amina.

231 Acha kulia, hapo, mama. Unamwombea rafiki aliye kwenye hospitali ya New Albany, aliye na TB. Uh-huh.

Je, mnaamini Yeye yupo hapa?

Vema, na tuviinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja sasa.

232 Roho Mtakatifu wa Mungu, wakati mwili wangu ukitetemeka, umetiwa mafuta na Uwepo Wako; sio wangu tu, bali wa wengine hapa ndani; Nguvu za kufufuka Kwako zinaishi miongoni mwetu sasa. Tunajua ya kwamba tunasimama mbele ya Mungu aliye hai Ambaye aliutikisa Mlima Sinai. Isitoshe, bali ataitikisa dunia katika Kuja Kwake, Yeye aliyemfufua Yesu katika wafu, naye amesimama hapa katika kanisa hili dogo usiku wa leo. Bwana, tusingeweza kujenga mahali panapostahili kutembelewa Nawe. Lakini, katika unyenyekevu Wako, Wewe umekuja palipo duni sana. Tunashukuru sana kwa ajili ya hilo. Umetutembelea. Umejithibitisha Mwenyewe miongoni mwetu.

233 Tunaliamini Neno Lako. Bwana, nimelinena, kama mtumishi Wako. Sasa jalia twendelee mbele, kama vile Ujumbe ulivyotuagiza. Jalia tusonge mbele, katika Nguvu za kufufuka Kwake. Jalia pasiwe na mtu mnyonge; jalia Roho Mtakatifu aingie kabisa kwenye jengo hili sasa na kumponya kila mtu aliye hapa. Jalia kusiweko na maradhi yoyote yaliyosalia miongoni mwetu. Jalia kusiweko na tashwishi hata kidogo miongoni mwa hawa watu. Jalia kuwe na mtikiso mkubwa sana miongoni mwa watu, sasa hivi, hata watajisikia ya kwamba mambo yote ni sawa. Lijalie, Bwana.

234 Wakati tumeviinamisha vichwa vyetu, ninataka mtu unayeketi karibu naye, ninakutaka wewe uweke mikono yako

juu ya mtu aliye karibu nawe. Weka tu mikono yako juu yao. Ndani ama nje, haijalishi uko wapi, wekeaneni mikono mmoja na mwenzake. Sijali unachohitaji. Hilo halijalishi hata kidogo. Sijali mtu huyo yuko wapi, huenda akawa ng'ambo ya bahari, ng'ambo ya bahari kuu. Haidhuru ni wapi, Mungu anafunika anga lote, anajaza wakati wote. Yeye yuna nguvu zote. Anaenea kila mahali. Yeye ni—Yeye hana kikomo. Yeye yuko hapa sasa. Anasikia maombi yako.

²³⁵ Biblia ilisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Na kila mmoja wenu ni mwaminio. “Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.”

²³⁶ Mmewekeana mikono. Mmeunganishwa hapa juu, kama kundi. Sasa ninawatakeni mwombeane. Omba kwa njia yako mwenyewe. Kila mmoja wenu aanze tu kuomba. Mwombee mtu mwingine, useme, “Bwana, mponye mtu ninayemwekea mikono.”

²³⁷ Bwana Yesu, wakati wakiomba, yasikie maombi yao, Bwana, wapate kujua ya kwamba si tu mtumishi mmoja. Wao ni watumishi Wako. Sisi sote ni mmoja. Tunakupenda, Bwana. Mahali petu mbalimbali, kanuni zetu mbalimbali za imani, madhehebu yetu kamwe hayatutenganishi na Mungu aliye hai. Sasa tuko Mbele Zake. Tunafurahia na kushukuru ya kwamba Wewe uko hapa. Hatustahili Uwepo Wako, bali tunaomba ya kwamba Wewe utayajibu maombi yetu. Tunafanya hili kulingana na Neno Lako. Wewe ulisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Nao wamewekeana mikono. Jalia Roho Mtakatifu mkuu Yule anayeweza kufunua siri za moyo, aliyeahidiwa na Biblia, Yesu aliye hai aliyefufuka ambaye aliahidi kuwa pamoja nasi hata ukamilifu wa dahari, mjalie sasa afanye kazi aliyoahidi. Tunakuamini Wewe, Bwana, tunapolikabidhi kusanyiko hili mikononi Mwako, katika Jina la Bwana Yesu Kristo. Amina.

²³⁸ Juu ya msingi wa mamlaka ya Neno lililoandikwa la Mwenyezi Mungu, kwa ushahidi wa Roho Mtakatifu Ambaye yuko hapa, anayezijua siri za moyo na kuwafunulia watu hizo siri; juu ya Uwepo Wake, msingi wa Neno la Mungu, ninamtangaza kila mmoja wenu, “ameponywa,” katika Jina la Yesu Kristo. Naomba muondoke wala msiwe wagonjwa tena. Mungu na awabariki na kuwalinda.

²³⁹ Natumaini kuwaona tena, hivi karibuni sana. Mpaka wakati huo, ibada inamrudia mchungaji, Ndugu Jackson. Mungu akubariki. 

59-1004E Mbona Unalialia? Nena!
Faith Assembly
Clarksville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org